**MAZUNGUMZO MAALUM**
Lissu ataja mambo matatu yanayomvutia utendaji wa Samia
UKURASA 4





**MWINYI** azindua bima maalum ya Kiislamu Zanzibar
UKURASA 17



ALHAMISI JULAI 6, 2023

ama AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12

Huu ndio ugonjwa sonona, Hospitali Sekou- Toure inavyopambana nao

MTAALAMU WA VETA Mbaazi, zao linalochuana na ngano kwa mambo mengi, lishe ikiwa juu

Ukurasa 14

Agizo la Samia; Pwani bila kuni, mkaa, operesheni imepamba moto

Na Khadija Kalili, Kibaha

• Ni angalizo alilotoa kuhamia gesi
• Makamba aanika ilikofika wizara

KITAIFA, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na serikali yake wako katika kampeni ya kutunza mazingira inayojumuisha kuondokana na utumiaji kuni na mkaa katika shughuli za jikoni.

Mnamo Novemba mwaka jana, Rais akaelekeza kuundwa kikundi kazi cha kupitia na kuchakata sera zilizopo, kuelekea kwenye mpango wa taifa kuondokana na matumizi ya gesi chafu kupikia, ifikapo mwaka 2032.

Ni maelekezo aliyoyatoa katika ufunguzi wa mjadala kitaifa kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Kikundi kiliochoundwa kinaongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Nishati, ikiratibu na kufanya shughuli za sekretarieti za kikundi hicho.

Ili kufikia tija na ufanisi, Rais Dk. Samia akaagiza kikundi kijumuishe wataalamu kutoka idara na taasisi za umma, sekta binafsi na wadau wa mazingira.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Dk. Selemani Jafo, akihamasisha wakazi kuacha kutumia kuni na kujikita kwenye gesi, katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ruvu, wilayani Kibaha mkoani Pwani. PICHA: MPIGAPICHA WETU.

Makamba anafafanua, mfuko utaweka ruzuku itakayowawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei ya gesi,: akihitimisha"...kazi kubwa, lakini inawezekana na 'Kazi Inaendelea'..."

Anaeleza kuwa serikali ya awamu ya sita imeamua kulivalia njuga suala la nishati safi, ikiwa ni katika jitihada zake za kuboresha maisha ya Watanzania, hasa kinamama.

Makamba anawarejea wasomi wa afya akitamka: "Wataalamu wanasema, saa moja jikoni ni sawa na sigara 300. Sasa hapa unategemea ustawi utatoka wapi? Bahati nzuri Mheshimiwa Rais, ameliona...."

PWANI YATEKELEZA

Ikiwa sehemu ya kuungana na Wizara ya Nishati, mkoa wa Pwani ukaandaa kongamano la siku mbili kujadili hoja ya kitaifa ya Nishati Safi ya Kupikia, ikiwa ni maelekezo na Dira ya Rais Dk. Samia, kuhamasisha matumizi ya nishati safi kupikia.

Ni mjumuiko wa washiriki 200 waliopatiwa mitungi ya gesi, ikiwa sehemu ya uhamasishaji nishati safi kupikia, wakiacha kuni na pia mkaa.

Inaendelea Uk. 14


UKURASA 11




# Nipashe
MWANGA WA JAMII
Alhamisi Julai 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581363
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


## Watafiti wabaini uchafu hewa Dar umezidi viwango vya WHO

*ANGALIZO lao; wakazi wako hatarini kwa magonjwa ya kupumua


UKURASA 2


# Udanganyifu NHIF, ndugu waoana wapate kadi tiba


UKURASA 2


## Lori lilivyoua 7 na kujeruhi 13 waokoaji ajali ya bajaji, bodaboda, gari


UKURASA 5




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mwanajiolojia wa Kampuni ya Mamba, Erasto Kafyullo, alipotembelea banda la Wizara ya Madini katika maonyesho ya Sabasaba, Dar es Salaam jana. **Habari kamili ukurasa wa 3 PICHA: JUMANNE JUMA**


**MICHEZO** YANGA YATAJA MASHARTI MATATU MAYELE KUONDOKA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba, akizungumza na wanachama wa mfuko huo waliotembelea banda la PSSSF kwenye Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NHIF yabaini udanganyifu wa ndoa batili kupata matibabu

**Na Abdallah Bakari,**
MTWARA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umebaini kuwapo udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wanachama na viongozi wa dini kwa kufungisha ndoa batili ndugu wa familia moja ili wakidhi vigezo vya kuwa mwanachama wa Mfuko huo kama mke na mume.

Hayo yalibainishwa jana katika mkutano wa wadau wa mfuko huo kwa Mkoa wa Mtwara, wakati Meneja wa Mkoa wa Mfuko huo, Dk. Adolph Kahamba, akiwasilisha taarifa mbele ya mkutano huo.

"Kuna tukio lilitokea nadhani vyombo vya habari vilitoa hapa Mtwara kwamba mtu amefunga ndoa na dada yake ili apate bima ya afya, kwa hiyo kumekuwa na udanganyifu na bahati nzuri viongozi wa dini mpo mtusaidie ili kuweka maadili."

"Ofisi yetu ina kesi shekhe ana 'confess' (kiri) bwana mimi kwa kweli nilidanganya nikafungisha ndoa ya uongo mtu na dada yake ili apate bima ya afya," alisema Dk. Kahamba.

**RIPOTI YA CAG**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), katika ripoti yake kwa mwaka 2020/21, mbali na mambo mengine, alibaini udanganyifu uliojumuisha wanaume 731 kuugharimu NHIF milioni ya shilingi kwa madai ya kupata huduma ya kujifungua kwa njia ya upasuaji.

Akizungumzia ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza, Dk. Kahamba alisema ulaji wa samaki wanaohifadhiwa kwa kuwekwa chumvi nyingi maarufu ng'onda huenda ikawa miongoni mwa sababu zinazochangia ongezeko la magonjwa hayo mkoani humo.

"Miaka mitatu iliyopita tulikuwa katika kampeni ya kuelimisha wananchi juu ya huduma zetu, wenzetu wa Hospitali ya Rufani ya St. Benedict pale Ndanda wakatuunga mkono kwa kutoa huduma ya vipimo vya magonjwa bure kwa wananchi, baada ya ile kampeni asilimia 32 ya waliopima waligundulika kuwa na magonjwa yasiyoambukiza bila ya wenyewe kujijua," alisema Dk. Kahamba na kuongeza;

"Kwa sasa mkoa wetu una wagonjwa 36 wa figo, kati ya hao 30 wanatibiwa kwa kutumia bima ya afya na sita wamepatiwa msamaha, maana yake wote hawa wanatibiwa na serikali, lakini wagonjwa wa BP, moyo ni wengi sana...magonjwa yanayotokana na mtindo wa maisha yetu yanaongezeka na ni aghali kuyatibia."

Alisema Mtwara kuna ulaji mkubwa wa chumvi, kutokana na samaki ng'onda wenye chumvi nyingi ambao huchangia kusababisha magonjwa yasiyoambukiza.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alibainisha kuwa hadi kufikia Machi 2023, watu 4.9 milioni sawa na asilimia nane ya Watanzania wote wamejiunga na Mfuko huo huku idadi ya Watanzania wanaopata huduma za bima ya afya ikijumuishwa na za kampuni binafsi imefikia asilimia 15.

Akizungumzia changamoto ya udanganyifu alisema "Kumekuwa na tatizo kubwa la udanganyifu kwa watoa huduma na wanachama hali iyonasababisha malipo hewa na kwa watu wasiostahili."

"Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) tumeamua kuingia katika mfumo wa utambuzi wa alama za vidole na picha ili kudhibiti udanganyifu kwa wanachama ambao huwapa kadi wagonjwa ambao siyo wanachama kwa lengo la kupatiwa matibabu bure."

Aidha, alisema magonjwa yasiyoambukiza ni mzigo kwa Mfuko huo kwa kuwa ugharimu fedha nyingi kuwatibia wagonjwa.

"Tazama Mfuko unatumia fedha nyingi kwa ajili ya wagonjwa wanaopata huduma za kuchuja damu, takribani Sh. bilioni 35 na dawa za saratani Sh. bilioni 22," alibainisha Konga.

Baadhi ya wadau waliushauri NHIF kushirikiana na wadau wengine kuelimisha umma kujikinga na magonjwa yasiyoambukizwa ndani ya Mkoa wa Mtwara ili kupunguza gharama za matibabu.

"Ni kweli ulaji wa chumvi huku Mtwara ni mkubwa, hii imekuwa kama mazoea sasa niombe NHIF ishirikiane na wadau wengine kuelimisha jamii kuepukana na matumizi makubwa ya chumvi na vichocheo vingine vya magonjwa yasiyoambukiza," alisema Filorgeus Manula, akichangia mjadala huo.

# Watafiti wabaini uchafu hewa Dar umezidi viwango vya WHO

**Na Beatrice Shayo**

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Chuo cha Mazingira Sweden, umebaini kuwapo uchafuzi mkubwa wa hali ya hewa mkoani Dar es Salaam uliovuka viwango vilivyowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Kutokana na hali hiyo, wataalamu hao wamependekeza kuwapo sheria kali na usimamizi mzuri wa mazingira ili kuondokana na uchafuzi wa mazingira hususani kwa njia ya hewa.

Mhadhiri wa DIT, Yasinta Manyele, katika jukwaa lililowakutanisha wadau wa mazingira wa ndani na nje ya nchi jijini Dar es Salaam juzi, alibainisha hali hiyo.

Manyele alisema utafiti huo ulifanywa kati ya Mei 2021 na Februari 2022, ukibainisha kuwapo uchafuzi mkubwa wa mazingira kwa njia ya hewa kupita viwango vilivyowekwa na WHO jijini Dar es Salaam.

Alisema utafiti huo ulifanyika kwa vyuo hivyo kuweka mashine maalum katika vituo 14 katika halmashauri zote za Dar es Salaam ili kubaini uchafuzi wa hewa ulioko.

Vifaa hivyo vilifungwa Uwanja Taifa, Shule ya Msingi Tabata, Shule ya Msingi Vigunguti, Shule ya Sekondari Jangwani, Dampo la Pugu na vingine vinne vilifungwa katika vituo vya mabasi yaendayo haraka (BRT), Hospitali ya Sinza Hospitali (Palestina) na Ofisi ya Mazingira Temeke.

Mhadhiri huyo alitaja madhara mojawapo yatokanayo na uchaguzi huo kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa magonjwa yanayohusiana na upumuaji.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Khamis Hamza Khamis, aliwaagiza washiriki wa jukwaa hilo kuja na mpango mkakati wa kuondoa tatizo hilo.

Alibainisha kuwa asilimia 80 ya uchafuzi wa mazingira mkoani Dar es Salaam unasababishwa na shughuli za kibinadamu ikiwamo ukataji miti, uchomaji mkaa, magari na kutumia nishati isiyo safi kupikia.

Khamis alitaka wajikite katika usimamizi, sheria na kanuni zinazohusiana na mazingira ikiwamo Sheria ya Mazingira ili kudhibiti tatizo.

Alisema elimu inahitajika kwa jamii ili kubadili mitazamo yao ili wapunguze uharibifu wa mazingira.

Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa Taasisi ya Uongozi, Degratias Usangira, alisema mkutano huo ulilenga kutoa matokeo ya utafiti uliofanywa na DIT na Chuo cha Stockholm Environment Institute Africa Centre cha Sweden, kuhusu ubora hewa mkoani Dar es Salaam.

Usangira alisema matokeo ya utafiti huo ni muhimu kwa sababu yatasaidia kuandaa mpango wa kusimamia ubora wa hali ya hewa mkoani hapa.

"Hii ni moja ya kazi ambayo tumeifanya, lakini tumekuwa na makongamano mbalimbali ya kuwaleta viongozi wa pamoja kwa ajili ya kujadiliana na kubadilishana mawazo," alisema.

Akizungumza baada ya kutembelea Shule ya Msingi ya Vingunguti, Mtafiti wa Masuala ya Ubora wa Hewa kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira ya Stockholm (SEI), Ngongang Danube, alisema ubora wa hewa (AQI) hupimwa na kipimo cha PM 2.5 na PM 10 na kiwango cha kimataifa cha hewa kinapaswa kiwe kati ya 0-50 ambayo ni nzuri.

Alisema kikiwa 50 hadi 100 bado iko kwenye kiwango kinachokubalika ingawa uchafuzi huo unaweza kusababisha athari za kiafya kwa wastani kwa idadi ndogo ya watu.

Danube alisema kifaa hicho katika shuleni ya msingi ya Vingunguti kilirekodi kiwango cha juu cha uchafuzi wa hewa hasa nyakati za jioni na usiku hewa inakuwa chafu zaidi na kufika hadi kiwango cha tahadhari ambacho ni zaidi ya 50.

Mtafiti Mwandamizi kutoka SEI, Dk. Romanus Opio, alisema uchafuzi wa hewa katika eneo hilo na mengine ya Dar es Salaam ni wa kiwango cha juu.

"Mfano kwa kifaa cha hapa Shule ya Msingi Vingunguti tulichofunga kimerekodi kiwango cha juu cha uchafuzi wa hewa. Hii ina maana wanafunzi wanaathirika kwa muda mrefu na uchafuzi huo mwingi ni kutoka viwanda vilivyo maeneo haya. Mamlaka zinapaswa kuchukua hatua," alitoa hadhari.

Dk. Opio alishauri ni vyema manispaa zikaweka sheria na kanuni za kufuatwa katika maeneo hayo ili viwanda vinavyochafua hewa zitakiwe kufunga vifaa vya kunyonya hewa chafu waitoayo kwa lengo la kupunguza athari kwa watoto na jamii inayozunguka maeneo hayo.

"Lakini mamlaka zisimamie na zivitake viwanda kutumia nishati mbadala ambazo ni rafiki wa mazingira. Hii itasaidia jamii isiendelee kuathirika," alishauri Dk. Opio.

Pia alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, ni muhimu kupanda miti mingi katika mipaka ya shule na taasisi za umma ili kaboni inayotoka viwandani inyonywe na miti kupunguza madhara kwa jamii inayozunguka viwanda hivyo.

Alishauri mamlaka na wadau wa mazingira waendelee kutoka elimu kuhusu utunzaji wa mazingira ili kuepukana na athari zake.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Vingunguti, Mfaume Ndumbaro, alisema kifaa hicho cha kupima uchafuzi wa hewa kimefungwa shuleni hako kusaidia kutambua kiwango cha hewa chafu iliyopo ili jamii ichukue tahadhari.

Alisema matokeo waliyopatiwa watakwenda kufanyia kazi ili wasiendelee kupata madhara zaidi kwa kuwa shule hiyo inazungukwa na viwanda vinavyosababisha uchafuzi wa hewa.

# PM: Machinga watengewe maeneo rafiki kibiashara

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesisitiza halmashauri zote nchini ukiwamo uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kuweka utaratibu wa kuwapanga wamachinga katika maeneo rafiki ili wafanye biashara zao kwa uhuru na kuchangia uchumi wa taifa.

Akizungumza jana katika hafla ya uzinduzi wa Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa maarufu Sabasaba, Majaliwa alisisitiza maeneo ya wamachinga yawekewe miundombinu muhimu, huku akitoa mfano soko la Dodoma jiji.



Alisema ni adhma ya serikali kutengeneza mabilionea kupitia biashara na kwamba ni fahari kwa nchi kuona wamachinga wanakua na kufanya biashara kimataifa, huku akimsisitiza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam lazima mkoa wake uwe na eneo la kufanya biashara saa 24.

"Pia nimefarijika kusikia kuwa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) wametenga eneo maalamu kwa ajili ya machinga kujifunza na kukua zaidi, niwasihi mjifunze mbinu mbalimbali za kibiashara ili muweze kukua zaidi," alisema na kuongeza;

"Mchango wa maonesho haya ni mkubwa katika kufungua masoko ya mazao, bidhaa zinazozalishwa viwandani na huduma zinazotolewa nchini machinga wayatumie kukua zaidi kibiashara kimataifa na Watanzania watembelee maonyesho haya kuwaunga mkono wafanyabiashara wetu," alisema Majaliwa.

**MAELEKEZO**

Waziri Mkuu, Majaliwa pia aliziagiza Idara ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara katika ngazi za mikoa na halmashauri zishirikiane na TanTrade kwa karibu ili kuhakikisha taarifa za uzalishaji wa mazao na masoko zinatolewa kwa wakati ili kuleta tija kwa wafanyabiashara.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara kufanya shughuli zao kwa kujiamini, weledi na uzalendo na kwa kuzingatia sheria kanuni na taratibu walizoziweka na watangaze biashara zao ndani na nje ya nchi.

"Mfanyabiashara yeyote mwenye maoni na ushauri wa namna ya kuboresha maonesho haya asisite kuyaleta milango iko wazi, pia kila anayeuza bidhaa atoe risiti na anayenunua adai risiti ili serikali ipate mapato na kuimarisha miundombinu yetu," alisema Majaliwa.

Hata hivyo, alitoa rai kwa taasisi zote za teknolojia kuwekeza katika kuzalisha wataalamu wengi zaidi katika eneo la gesi asilia ili kuwasaidie kupunguza kasi ya uchafuzi wa mazingira.

Vile vile, alitoa wito kwa wizara za uwekezaji viwanda na biashara Bara na Zanzibar kuweka mpango shirikishi na wizara za kilimo ili kuandaa mipango pamoja na wahakikishe inafanyika kwa kuzingatia mahitaji ya soko ya ndani na nje.

"Wizara hizi mbili lazima zisomane kiutendaji na TanTrade ishirikishe wizara hizo katika utekelezaji na ufungaji wa bidhaa na kutafuta fursa ya masoko ndani na nje ya nchi, huku akiwasisitiza wafanyabiashara na wazalishaji wa bidhaa kutumia teknolojia kupunguza gharama uzalishaji ili kuwa na bei shindani sokoni.

Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Latifa Khamis, alisema maonyesho hayo ni moja ya nyenzo muhimu inayotumika kutangaza bidhaa za Tanzania, kuwakutanisha wafanyabiashara wa ndani na nje kujifunza na kubadilishana uzoefu wa biashara.

Naye Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema katika kuimarisha uwekezaji na biashara nchini, bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 wameweka vipaumbele mbalimbali vinavyokusudia kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji na kuvutia wadau wa ndani na nje ili kukuza uchumi.

# Serikali yashtuka fedha mbichi bilioni 1.6/- ziko hatarini kuliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Adolf Ndunguru, amewaagiza makatibu tawala wa mikoa kwenda kushughulikia fedha mbichi Sh. bilioni 1.6 zilizoko katika baadhi ya halmashauri na kuhakikisha zinaingizwa benki.

Ndunguru alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipofunga kikao kazi cha siku mbili cha kutambua mafanikio na kero zilizojitokeza katika utekelezaji wa Programu ya Mifumo katika Sekta ya Umma kwa baadhi ya watendaji wa mikoa.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23 uliofika ukomo Juni 30 mwaka huu, zipo baadhi ya halmashauri ambazo hazijamaliza kazi ya usuluhishi wa hesabu zake na zingine zimeendelea kubaki na fedha mbichi.

"Tunapofunga mwaka, tuna takribani Sh. bilioni 1.6 hazijapelekwa benki, bado mnazo mikononi. Ninawasihi mwende mkawasimamie wakurugenzi wahakikishe fedha hizo kwanza, wakamilishe usuluhishi wa hesabu. Wahakikishe fedha hizo mbichi ambazo bado wanazo mikononi zinakwenda benki," aliagiza.

Alisema ofisi yake itaendelea kutoa ushirikiano wa hali juu kwa mradi wa PS3+ ili kuendeleza na kuimarisha mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika mikoa.

Ndunguru alisema Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi zilizo chini yake kama ilivyo kwa vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi na elimu. Ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji katika utoaji huduma bora kwa wananchi unahitaji.

# PSSSF kuwalipa wastaafu wao bila kufika ofisini

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi (PSSSF), Hosea Kashimba, amesema wanatarajiwa kuzindua mpango mpya ndani ya miezi miwili ijayo ili mstaafu apatiwe huduma ya malipo yake bila kufika ofisini kwao.

Kashimba aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari katika banda lao la PSSSF kwenye Maonesho ya Biashara ya 47 Kimataifa yanayoendelea kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.

"Tunarahisisha namna ya kumhudumia mwanachama, hivi karibuni tutazindua mpango ndani ya miezi miwili ijayo yaani mwanachama akiwa amekaa nyumbani kwake au sehemu yoyote amekaribia kustaafu ama amestaafu anajaza fomu kwenye kompyuta na mwajiri wake anaiona anaituma kwetu sisi tunaifanyia kazi hela anaikuta benki," alisema Kashimba.

Pia alisema mpango huo utamwondolea mwanachama usumbufu labda ikitokea ana shida nyingine ambayo inamlazimu kufika ofisi ya PSSSF.

"Timu yetu itakapofika kwa waajiri kufanya mafunzo na elimu kwa wanachama kama ana swali atapata majibu pia anaweza kutupigia kwa simu tukamsaidia tunaenda kidijitali," alisema Kashimba.

Aidha, Kashimba alisema biashara ya majengo ina lenga kuweka thamani fedha na uwekezaji wao unaenda vizuri kuna changamoto ilitokea wakati wa Uviko-19.

Alisema siyo kweli kwamba miradi yao ipo kwenye hali mbaya, Rais Samia Suluhu Hassan amefungua uchumi wa nchi na kuna wawekezaji wengi wameingia nchini."Mtikisiko ulitokea hapo katikati kutokana na Uviko-19 watu wakafunga biashara na kwa sasa tunaona dalili njema na majengo yetu yameanza kupata wateja hasa kwenye makazi ya watu," alisema Kashimba.

Alisema kwa wastani wa majengo yao ya mfuko yapo asilimia 75 na wamepewa fursa ya kuwekeza zaidi katika maeneo ya hati fungati.

Vile vile, wanaangalia maeneo yenye fursa ili kufanya uwekezaji na hali ya mfuko ipo vizuri na wanalipa mafao kwa wakati.

"Ndani ya siku 60 tunalipa mafao kwa wanachama wetu hiyo ndio tathmini halisi ya hali ya mfuko wetu tuna thamani ya Sh. trilioni 8.3," alisema Kashimba.

Aidha, aliwataka wateja kutembelea banda lao ili waweze kupatiwa huduma yoyote wanayoitaka na kama wamekutana na changamoto itatatuliwa.

Alisema jambo la muhimu ni wastaafu kuwa makini na fedha zao ili kuepuka kutapeliwa kutokana na baadhi yao kujikuta wakifanyiwa uhalifu na matapeli.

Kashimba alisema mfumo wa PSSSF utaendelea kutoa elimu kwa wanachama wake ili fedha zao zibaki kuwa salama.




MAZUNGUMZO MAALUM



Mkuu wa Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, Jokate Mwegelo (katikati), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Araman Bonoite (wa pili kulia), wakimkabidhi mtungi wa gesi ya Oryx na jiko mjumbe wa Kikundi cha Lutind Tea Herbs and Spices, Mariam Isidor jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tundu Lissu ataja mambo matatu yanayomvutia utendaji wa Samia

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu,ametaja mambo matatu yanayomfanya avutiwe na utendaji wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Lissu ameiambia Nipashe wiki hii kwamba mambo hayo yanajumuisha kurejeshwa kwa diplomasia nchini, anayodai ilikuwa imevurugika, kuonyesha tabasamu kwa upinzani na anachokiita kuondolewa 'kamatakamata' ya viongozi na wafuasi wao.

"Anatabasamu sana na hatutukani kirejarejа..." anatamka Lissu, japo anageukia upande wa pili wa shilingi, akikosoa mambo kadhaa katika uongozi wa sasa, akibainisha hakubaliana nayo.

"Anazungumza mapatano, mapendano, maridhiano ingawa sasa kwenye vitendo hajafanya hata moja," amesema Lissu.

Pia Lissu amemkosoa Rais Samia katika kile anachodai, kwa baadhi ya uteuzi wake wa watendaji wa ngazi za juu kiserikali, hakubaliani nao huku akitoa orodha ya nafasi kadhaa.

Vilevile, Lissu ambaye katika mazungumzo hayo na Nipashe mkoani Dar es Salaam alikuwa mwazi zaidi, akikiri kuwapo tofauti ya kiitikadi na kaka yake, Alute Mungway, ambaye ni mwana CCM, akidokeza anaheshimu tofauti hiyo.

Kwa mujibu wa Lissu, bado kaka yake huyo ambaye naye ni mwanasheria mwandamizi kama alivyo yeye, anamtaja ni mwalimu wake wa kimaisha, akieleza mahususi katika fani ya sheria, amechangia mzizi wake kumea.

"Sisi ni watu wawili tofauti, tumetoka katika tumbo moja, lakini ni watu wawili tofauti. Kaka yangu ni mwana CCM, japokuwa mimi ninajua CCM anayoifuata kaka yangu haijawahi kuwapo, lakini yeye ukimwuliza, atakwambia ni mwana CCM," amesema Lissu. Mwanasiasa huyo anamsifu kaka yake, akitumia kauli: "Na mimi siyo mwana CCM, kwenye hilo tunatofautiana kama binadamu wawili tofauti. Tofauti za mtazamo ni vitu vya kawaida.

"Lakini huwa ninapenda kusema kuwa, kama asingekuwa yeye, mimi ningeenda kusoma sheria na nimeisema hiyo miaka yote, nitaisema leo na kesho, ni wanasheria wachache ninaoweza kusema huyu 'ameni-inspire' (amenivutia), Alute ni mmojawapo."

**CHADEMA NA GHARAMA**

Katika nafasi yake ya uongozi wa chama, Lissu amewека wazi namna operesheni zao, ikiwamo 255 Katiba Mpya wanayozunguka nchi nzima kuhamasisha shinikizo kwa serikali kuridhia rai yao, wanaelemewa na gharama kubwa.

Lissu amesema bajeti ya operesheni hiyo ni kubwa maradufu kuzidi ruzuku Sh. milioni 109 wanayopata, hata wanalazimika kuchangisha wanachama na wadau wengine wanaojitolea kukijenga chama.

**KILIO CHA AJIRA**

Lissu pia amezungumzia kilio cha uhaba wa ajira, hususani kwa vijana nchini, akisisitiza kunahitajika kubadilisha sera na mfumo wa kiuchumi.

Amesema mfumo uliopo sasa hauwezeshi kuzalishwa ajira za kutosheleza mahitaji yaliyopo nchini, vyuo vikuu vikizalisha zaidi ya wahitimu 100,000 kila mwaka.

Mwanasiasa huyo amesema tatizo la sera na mfumo wa uchumi analodai huamuliwa na viongozi wa kisiasa, lina athari za moja kwa moja katika kuzalisha ajira kwa vijana nchini.

"Uhaba wa ajira ni tatizo la mfumo wa uchumi na ni tatizo la kisiasa na sera kwa sababu sera ni siasa, zinaamuliwa na wanasiasa, kutakuwa na wataalamu lakini wanaofanya uamuzi ni serikali.

"Uchumi wetu ni wa aina ambayo haitengenezi ajira za kutosha. Tunahitaji sera za kiuchumi ambazo zinaweza zikatengeneza ajira za kutosha," amesema.

Kwa mujibu wa Lissu, suala hilo linahitaji mfumo mpya wa kiuchumi, sera na aina mpya ya siasa ili kuleta matokeo tofauti na ilivyo sasa.

"Nikupe mfano tu, nimekwenda Kanda ya Magharibi, mikoa ya Kigoma na Katavi. Hiyo mikoa mitatu ambayo nimeitembelea, kimsingi ukiingia Tabora kuanzia hapa Shelui ukienda na hiyo barabara, ukapita Shinyanga, ukapita Geita ukaenda Kigoma ukatoka huko Katavi, ukarudi Tabora...

"Hiyo mikoa ukipita barabarani utaona kwamba inaweza kuzalisha mpunga ukalisha Afrika Mashariki na Kati kwa mpunga utakaotoka katika hiyo mikoa na watu wanalima sana.

"Lakini sehemu ambayo wanalima kulinganisha na sehemu ambayo wanaweza kulima ukiwa na sera sahihi ni kubwa sana.

"Nilikutana na bwana mmoja akaniambia kwamba yeye na wanakijiji wenzake wanataka waanzishe mradi wa umwagiliaji ambao wakiwa na Sh. milioni 700 wanaweza wakatengeneza hekta 15,000 za mpunga.

"Karibu na hilo eneo, kuna mradi wa serikali ambayo imetengeneza hekta 5,000 na imetumia Sh. bilioni mbili hivi. Alinipa hesabu fulani ya ajabu kwelikweli. Yeye anasema 'tukiwa na Sh. milioni 700 tutatengeneza hekta 15,000 za mpunga'. Sasa haya ni mambo yanayohitaji sera sahihi na siasa sahihi," Lissu amesema.

Kuhusu ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuwa na 'madudu' yanayojirudia kila mwaka, Lissu amesema ni suala la kimfumo, akidai mfumo wa uongozi wa sasa hauwafanyi viongozi kuwajibika kwa wananchi moja kwa moja na kwa hivyo hakuna hofu kiongozi kuiba mali ya umma.

"Tunahitaji mfumo mpya wa namna ya kuendesha nchi yetu. Mfumo uliopo wa kikatiba na wa kiutawala wa nchi yetu, hauna uwajibikaji wowote kwa mtu yeyote mwenye madaraka yoyote katika ngazi yoyote.

"Ni mfumo ambao umejengwa kwa Rais ambaye ni... (alitaja neno linalohitaji uthibitisho kisheria). Na kwa hiyo, wa chini yake wote wanakuwa ni miungu watu kwenye nafasi zao. Hakuna uwajibikaji.

"Kwa hiyo, ukitaka kuwe na uwajibikaji na rasilimali za nchi zitumike sawasawa, inabidi kuweka uwajibikaji katika mfumo wa utawala," Lissu ameshauri.

Amesema kuwa nchi inapaswa kuweka mfumo mzuri wa uwajibikaji ili kuwashughulikia viongozi wakubwa wa serikali, mashirika na taasisi za umma pale inapogundulika wamefanya ubadhirifu katika maeneo wanayoongoza, kiutawala au kijinai. Amedai mfumo wa sasa umejaa kinga kwa wakosaji hasa walioko madarakani.

## Othman awataka madaktari kutoa huduma bora kwa jamii

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka madaktari na wahudumu wa afya nchini kutoa huduma bora kwa jamii ili juhudi za serikali za kusaidiana na wahisani wa maendeleo katika kuimarisha huduma za afya ziweze kuleta tija zaidi kwa wananchi.

Othman aliyasema hayo Kizimkazi Dimbani, Mkoa wa Kusini Unguja, alipokuwa akiweka jiwe la msingi la Kituo cha Afya cha Mama na Mtoto kilichojengwa na wahisani kutoka Oman ikiwa ni juhudi za serikali za kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya Zanzibar.

Othman alisema kufanya hivyo pia ni kuonesha kivitendo kuithamini misaada ya maendeleo inayotolewa na wahisani mbalimbali katika kuunga mkono juhudi za serikali za kuimarisha huduma kwa wananchi wake.

Alisema afya ya mtoto anayeweza kuwa na makuzi bora na akili imara inaanza katika hatua ya upatikanaji wa huduma na lishe bora kwa mama na ni muhimu kwa wahudumu wa afya kujitahidi kuendeleza utoaji wa elimu ya afya kwa mama.

Alisema taifa linahitaji vijana wenye siha na afya bora inayotokana na mama kuwa na lishe sahihi na kumnyonyesha ipasavyo mtoto tangu hatua ya awali ya kuzaliwa ili kuijenga misingi ya afya yake kwa mujibu wa taratibu za kitaalamu.

Aliwataka wazazi nchini hasa kinababa kuzingatia ipasavyo muda wa mtoto kupata haki ya kunyonya maziwa ya mama jambo litakalomwezesha kuwa na afya bora, makuzi imara na hatimaye kupata akili bora.

Alisema ni wajibu wa wananchi na watumishi wa afya kushirikiana na kuviona vituo hivyo vya afya siyo mali ya wizara ama serikali bali wavichukulie ni mali yao kwa kuweka ushiriki wao ipasavyo katika kuvitunza ili viweze kudumu na kutimiza malengo ya kuleta huduma zenye tija kwa wananchi.

Othman aliwataka wananchi kuacha tabia ya kula vyakula vya viwandani kwa kuwa ni miongoni mwa mambo yanayoweza kuleta changamaoto kubwa ya afya ndani ya jamii huku serikali ikifanya kila juhudi kuzifanyia kazi changamoto zilizopo kwenye sekta hiyo.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kwamba serikali kupitia wizara hiyo inafanya kila juhudi kuhakikisha huduma za afya kwa jamii nchini zinaimarika ipasavyo ili kufikia malengo ya dunia.

Kadhalika kutokana na hatua hiyo serikali, ifikapo Januari 2024, inakusudia kuifanyia matengenezo makubwa Hospitali ya Rufani Mnazimmoja mjini Zanzibar ili iweze kuwa na hadhi na kuwa na kiwango cha kisasa cha utoaji wa huduma nchini.

Naye Mfadhili wa ujenzi wa kituo hicho kilichogharimu zaidi ya Sh. milioni 77, amesema hatua hiyo ni mwanzo wa mwendeleo wa kuisaidia Zanzibar katika upatikanaji wa huduma kwenye sekta hiyo.

# Wanaume mkoani Njombe wahamasika kupima VVU

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, amesema wanaume 31,372 wamepima Virusi vya Ukimwi (VVU) mkoani Njombe huku 874 wakigundulika kuwa na maambukizi na kuunganishwa katika huduma ya tiba na matunzo.

Ummy aliyasema hayo wakati akipokea taarifa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe kuwa mafanikio hayo ni kutokana na kampeni ya Furaha Yangu ambayo ilikuwa inahamasisha wanaume kupima.

"Tunafahamu huko nyuma mwamko wa kupima wanaume ulikuwa chini, lakini tunashukuru Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa kufanya programu maalumu ya kampeni inaitwa Furaha Yangu ya kuhamasisha wanaume kujitokeza kupima kwa hiyo nawashukuru kwa sababu mmeitikia wito," alisema Ummy.

Alitoa wito kwa wanaume nchini kuendelea kupima ili kufahamu afya zao na wakikutwa na maambukizi wasiogope watumie dawa.

"Dawa zipo na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na serikali yake sikivu inaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba tunanunua dawa za kuwapatia waathirika wa virusi vya Ukimwi na dawa zile ni bure kwa hiyo mtu asije akafikiri ni hela, hapana dawa zile ni bure unapewa na bahati nzuri watu wetu Wizara ya Afya na TAMISEMI tumejipanga vizuri kuhakikisha tunawahudumia, lakini tunawapa ushauri nasaha wanaokutwa na maambukizi," alisema Ummy.

Aidha, aliwataka waratibu wa Ukimwi Mkoa wa Njombe kushirikiana na mashirika ili kutoa elimu kwa kundi la vijana ili lisiachwe nyuma. "Pia naomba katika mapambano haya msiwasahau wazee na watu wenye ulemavu kuhakikisha wanashirikishwa kwa sababu suala hilo ni mtambuka linahitaji juhudi za kila mtu," alisema Ummy.

Akisoma taarifa kwa Naibu Waziri, Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Dk. David Ntahindwa, alisema kuwa mkoa umefikia wanaume 31,372 na wanawake 45,373 kwa huduma ya upimaji, kati yao wanaume 874 sawa na asilimia 2.8 na wanawake 1,595 sawa na asilimia 3.5 waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU na kuunganishwa katika huduma ya tiba na matunzo.

# Ajali yaua saba, yajeruhi 13

**Na Moses Ng'wat,** TUNDUMA

WATU saba wamefariki dunia na wengine 13 kujeruhiwa baada ya lori kuwaparamia na kuwagonga wakati wakimsaidia kumnasua dereva wa bodaboda aliyeingia chini ya lori lingine lililomgonga eneo la Mpakani, mjini Tunduma, wilayani Momba.

Mashuhuda wa ajali hiyo waliiambia Nipashe kuwa baada ya dereva huyo wa bodaboda kugongwa na lori aina ya Fuso (IT), abiria waliokuwamo kwenye bajaj waliokuwa wakipita eneo hilo, waliteremka kuungana na wananchi wengine waliokuwa wanapita njia kumsaidia kumnasua chini ya Fuso hilo.

Walisema wakati wakiwa kwenye harakati za kumnasua, ndipo lori lingine lililokuwa linapita eneo hilo lilishindwa kufunga breki na kuligonga lori lingine lililokuwa limepakia mchanga na kwenda kuwagonga watu hao.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopister Mallya, magari yaliyohusika kwenye ajali hiyo ni malori matatu, bodoboda, gari dogo aina ya Hiace na bajaji,

Alisema, baada ya tukio la lori kugonga kundi hilo la watu, liliendelea kugonga magari mengine likiwamo gari dogo aina ya Hiace lililokuwa na abiria.

Kamanda Mallya, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana saa 12:45 mchana katika eneo hilo.

Alisema watu watano walifariki dunia papo hapo na wengine wawili wote wanaume walifariki dunia wakati wakiendelea kupatiwa matibabu Kituo cha Afya Tunduma.

Alisema kati ya majeruhi 13 waliopokewa kituo hicho cha afya, 10 walitibiwa na kuruhusiwa.

"Kati ya watu hao saba (wote wanaume) waliofariki, sita wametambuliwa na ndugu zao na miili yao imehifadhiwa katika kituo hicho cha afya," alisema.

Waliofariki na kutambuliwa na ndugu aliwataja kuwa ni Baraka Mwankenja (25), maarufu kama Fally Ipupa ambaye ni dereva wa bodaboda, Isaac Kasebele (28), Baraka Lutufyo (23), Fred Karagwe (28), Emmanuel Mlay (24) na John Kapizo (25), wote wakazi wa Tunduma.

Kamanda aliwataja majeruhi wanaoendelea na matibabu ni Zainab Hassan (43), Oliva Ngusa (38), Hassan Kwambaza (45), dereva wa lori.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati), akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Mwada Kata ya Magugu wilayani Babati, baada ya ziara yake ya kukagua ujenzi wa Shule mpya ya Msingi Melkiroy juzi. **PICHA GIFT THADEY**

# NBAA yaonya vishoka uhasibu, ukaguzi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

BODI ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) imewaonya vishoka wanaofanya shughuli za uhasibu na ukaguzi bila kufuata utaratibu, itachukua hatua dhidi yao kulingana na vigezo vya taaluma.

Mkurugenzi Mtendaji NBAA, Pius Maneno, alitoa onyo hilo jana mjini hapa wakati wa uzinduzi wa taasisi ya vijana inayojihusisha na masuala ya kutoa elimu ya uhasibu na ukaguzi ya SUYOO Group.

Katika risala yake iliyosomwa na Ofisa Elimu na Mafunzo NBAA, Sawa Ngendabanka, Maneno alisema kuna utaratibu unaofanywa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha wanachukuliwa hatua ikiwamo kufungiwa vyeti vyao kwa vigezo vya taaluma vilivyowekwa.

Kiongozi huyo pia aliwataka vijana wanaochipukia kuingia kwenye taaluma ya uhasibu na ukaguzi, kujenga imani nayo kwa sababu ina nafasi kwao ya kuajiriwa au kujiajiri. Alisema serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali zikiwamo za kuwaondoa kazini wahasibu na wakaguzi wanaokiuka sheria za NBAA, miongoni wakiwa ni vishoka wa taaluma.

Alisema fani hiyo husaidia taifa katika kutengeneza miongozo ya kihasibu ambayo inatumika pia kimataifa na kufanya wepesi wa mkaguzi kugundua mapema kama mwongozo haukufuatwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni inayojihusisha na utoaji wa mafunzo ya taaluma kwa bodi za wahasibu na wakaguzi Tanzania (SUYOO Vijana Group), Suka Machomanne, aliwataka wahasibu na wakaguzi kuendeleza mafunzo katika kituo cha shahada ya uhasibu kilichoko Shule ya Sekondari Morogoro.

Kuhusu vishoka, alisema mambo hayo hutokea kwa sababu vijana wengi wanamaliza vyuo na baadhi yao kukosa ajira na wengine wanakuwa hawajafikia viwango vya kusajiliwa kimkataba.

Aliwakumbusha wale ambao wanafanya shughuli hizo bila kutambuliwa wanakiuka maadili ya uhasibu na ukaguzi.

Mwanafunzi wa ukaguzi na uhasibu kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM), Dhaidi Swalehe, alisema kampuni hiyo itasaidia wanafunzi kupata nafasi ya kujifunza na kwenda kufanya mitihani ya bodi na kuwa wahasibu wazuri.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Watanzania tukienzi, tujivunie Kiswahili*

**KESHO** ni Siku ya Kiswahili Duniani na Watanzania wana kila sababu ya kujivunia lugha hii adhimu inayowatambulisha katika mataifa mbalimbali.

Lugha ya Kiswahili kwa sasa inazungumzwa na nchi nyingi duniani na inatoa fursa kubwa ya ajira kwa Watanzania kwenda nje ya nchi zinazojifunza lugha hiyo kwenda kufundisha.

Tumeshuhudia raia wa nchi za Ulaya, Marekani, Asia na baadhi ya nchi za Afrika zinazozungumza lugha hiyo, wakiongea kwa ufasaha na kuifurahia.

Maadhimisho ya Pili ya Siku ya Kiswahili Duniani yanafanyika katika kipindi ambacho BAKITA inatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kubidhaisha Kiswahili (2022/23 - 2031/32). Mkakati huu umeandaliwa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), chini ya usimamizi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya Zanzibar.

Mkakati huu ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango Julai 7, 2022 wakati wa Maadhimisho ya Kwanza ya Siku ya Kiswahili.

Maeneo ya kipaumbele yanayoshughulikiwa katika utekelezaji wa mkakati huo ni pamoja na uuzaji wa taaluma za Kiswahili, ukuzaji na uimarishaji wa miundombinu ya kufundisha na kujifunzia Kiswahili, uuzaji wa machapisho ya Kiswahili, uuzaji wa rasilimaliwatu na uuzaji wa huduma mbalimbali za Kiswahili kama vile tafsiri, ukalimani, uhariri, ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni na makundi mengine yanayohitaji, uandishi, utangazaji na ukuzaji wa sanaa ya Tanzania.

BAKITA limeendesha mafunzo ya kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa Watanzania wanaoishi katika nchi mbalimbali duniani pamoja na kuwafundisha baadhi ya wananchi wa nchi hizo waliotamani kujifunza lugha hiyo.

Miongoni mwa nchi zilizotembelewa na wataalamu wa BAKITA kwa ajili ya mafunzo hayo ni Malawi (Novemba, 2022), Burundi (Desemba, 2022) na Nigeria (Mei 2023). Nchi nyingine zilizopatiwa mafunzo hayo ni Falme za Kiarabu za Abu Dhabi na Dubai, Italia, Uholanzi, Zimbabwe na Rwanda (Juni, 2023).

Wakati wa maandalizi ya maadhimisho hayo, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesisitiza umuhimu wa kuzingatia matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili hasa katika vyombo vya habari.

Wahariri wa vyombo vya habari wametakiwa kuchukua nafasi ya kulinda lugha hiyo ili kuepusha upotoshaji ambao utaathiri maendeleo ya lugha hiyo kwa kizazi kijacho.

Matumizi sahihi na sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa yatafungua nafasi na fursa kwa vijana mbalimbali kupata ajira katika lugha hiyo nje ya nchi.

BAKITA na BAKIZA zimepewa changamoto ya kufanya utafiti zaidi katika kukuza lugha ya Kiswahili.

Utafiti huo ni muhimu kwa ajili ya kukiendeleza Kiswahili na kuwa miongoni mwa lugha maarufu inayotumiwa na watu wingi duniani kote.

Mpaka sasa jumla ya vyombo vya habari vya utangazaji redio 38 duniani vinarusha matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili, hivyo ni vyema waandishi wa habari wakaitumia fursa hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

### Muungwana Lazima Nilonge

## *Kwa tatizo hili la afya ya akili, visu, mapanga visiuzwe holela*

**INAKADIRIWA** watu milioni saba wana ugonjwa wa afya ya akili nchini, huku takwimu zikionyesha kuwa mwaka 2021 walioathirika na aina mbalimbali za magonjwa ya akili duniani walikuwa takriban milioni 970.

Inaelezwa, magonjwa hayo yanahusisha sononа, wasiwasi, kizofrenia na magonjwa ya akili kwa watoto na vijana na kwamba kati yao, watu milioni 301 wanasumbuliwa na ugonjwa wa akili aina ya wasiwasi.

Wakati watu hao milioni 301 wakiwa katika hali hiyo, wengine milioni 280 wana ugonjwa wa akili aina ya sononа na kwamba wanawake huwa wanaathirika zaidi kuliko wanaume kwa asilimia 52.4.

Hayo yamo kwenye taarifa ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, wakati akifungua semina kwa wahariri wa vyombo vya habari katika kuadhimisha Wiki ya Afya ya Akili jijini Dar es Salaam.

Vilevile inaelezwa kuwa, mtu mzima mmoja kati ya wanne anapitia ugumu wa afya ya akili, pia mtu mzima mmoja kati ya watano mahali pa kazi, anapitia matatizo ya afya ya akili.

Sababu za tatizo la afya ya akili, zinatajwa kuwa ni mtu kushindwa kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha, vinasaba, vilevi, magonjwa ya mwili kama vile UKIMWI na malaria kali.

Mbali na sababu hizo, nyingine ni msongo wa kiwango cha juu, shinikizo la makundi rika na matukio yenye tishio la maisha kama vile majanga, ukatili, unyanyasaji na migogoro.

Nimetoa maelezo marefu kidogo, lakini hoja yangu ni kwamba, ugonjwa huo upo, basi ni vyema tahadhari mbalimbali zikachukuliwa, ili ugonjwa huo usisababishe madhara kwa wengine.

Kwa kuwa mtu akiwa na msongo wa mawazo unaotokana na hilo tatizo la afya ya akili anaweza kufanya tukio lolote baya, basi ni vyema mtindo wa sasa wa kuuza vitu hatari kiholela ukadhibitiwa.

Hapa ninaaminisha uuzwaji wa mapanga na visu kiholela mitaani, mtindo ambao kwa sasa unaonekana kama wa kawaida, lakini ninadhani unaweza kusababisha madhara makubwa tahadhari zisipochukuliwa.

Ninadhani ipo haja kwa serikali kuangalia upya mtindo huo, kwani inawezekana mtu mwenye tatizo la afya ya akili akipita katika mkusanyiko wa watu na kupora silaha na kuanza kujeruhi wengine.

Kwa wakazi wa Dar es Salaam ninaamini watakuwa wameshuhudia uuzwaji wa silaha hizo kwenye mkusanyiko wa watu, kitendo ambacho akitokea mwenye tatizo hilo anaweza kusababisha makubwa.

Ni wazi kwamba katika karne hii yenye kesi za tatizo la afya ya akili inaogopesha kuona visu, mapanga na vinginevyo vinaruhusiwa kuuzwa waziwazi barabarani tena hata bila kuwekwa katika mifuko yake.

Wakati mwingine wauzaji wa silaha hizo huwafuata madereva, hasa katika maeneo yenye taa za kuongozea magari na kuwaonyesha silaha hizo kupitia dirishani kitendo ambacho ninadhani nacho ni hatari.

Inasikitisha kusikia kwamba nusu ya magonjwa yote ya akili duniani yanaanza katika umri wa miaka 14 na mengi ya hayabainiki wala kutibiwa, hali ambayo inatatanisha mustakabali wa vijana wengi.

Aidha, imekuwa ikielezwa kuwa mzigo wa matatizo ya akili miongoni mwa vijana unasababisha mambo makubwa matatu ambayo ni msongo wa mawazo, kujiua ikiwa ni sababu inayoshika nafasi ya pili kwa vifo vya vijana kati ya umri wa miaka kutoka 15 hadi 19 na tatizo linaloongoza ni matumizi mabaya ya pombe na mihadarati.

Wakati hali ikiwa hivyo, ni vyema silaha kama hizo zisiuzwe hadharani kuepusha madhara zaidi, kwani inaweza kuwa rahisi kwa mtu mwenye tatizo hilo kuichukua na kudhuru wengine au kujidhuru.

# Fundi mwashi kizimbani kwa tuhuma ubakaji mwanafunzi

**Na Grace Gurisha**

FUNDI mwashi, Noel Malisa, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, akikabiliwa na tuhuma za kumbaka mwanafunzi mwenye umri wa miaka 16 (jina tunalihifadhi).

Akisoma hati za mashtaka, Wakili wa Serikali Magreth Makinge, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Nestory Baro, alidai mshtakiwa anatuhumiwa kwa mashtaka ya kubaka.

Wakili Magreth alidai kuwa katika tarehe isiyojulikana Desemba 2022, mshtakiwa akiwa eneo la Kitunda jijini Dar es Salaam, anatuhumiwa kumbaka mwanafunzi huyo.

Mshtakiwa ambaye ni mkazi wa Kitunda baada ya kusomewa shtaka hilo, alikana kuhusika na tuhuma hizo zinazomkabili.

Upande wa mashtaka ulidai upelelezi haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Baro aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 31, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi zilipofikia.

# Benjamin Mkapa, NBC kusomesha wakunga 100

**Na Joseph Mwendapole**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imeungana na Taasisi ya Benjamin Mkapa kuanzia mpango wa kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafuzi wa taaluma ya ukunga nchini ili kuunga mkono juhudi za kupambana na changamoto za vifo vinavyotokana na uzazi kwa wanawake.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea na kukabiliwa na upungufu wa wafanyakazi wa kuwahudumia wajawazito, jambo ambalo husababisha vifo vingi.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2020, karibu asilimia 95 ya vifo vya wanawake wajawazito vilitokea katika nchi zinazoendelea huku idadi ya vifo hivyo kwa Tanzania ikiwa juu.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji sahihi, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC Theobald Sabi, alisema ushirikiano kati ya NBC na Taasisi ya Benjamin Mkapa ni wito wa wadau kuungana katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo.

Alisema kupitia ushirikiano huo, NBC itatoa ufadhili wa masomo kwa wakunga na hivyo kuboresha huduma kwa wajawazito lengo likiwa ni kupunguza vifo vinavyoepukika.

Alisema NBC inayofuraha kutoa mchango wake katika kusaidia kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

"Tukiwa kama benki inayothamini ustawi wa jamii tunajivunia kutoa mchango wetu kusaidia maendeleo ya jamii ambayo tunaihudumia. Tunafahamu umuhimu na uharaka wa kushughulikia suala la vifo vinavyotokana na uzazi hapa nchini na tunaamini uwekezaji kwenye elimu na mafunzo kwa wakunga wetu kutasaidia sana kupunguza vifo vinavyoweza kuepukika," alisema.

Alisema ni furaha kwa benki kutoa sehemu ya kiasi kinachopatikana kutokana na uchangishaji fedha wa kila mwaka kupitia mbio za NBC Dodoma Marathon na kuzielekeza kwenye utatuzi wa chagamoto hiyo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Benjamin Mkapa, Dk. Ellen Mkondya, aliishukuru benki hiyo na kuwataka wadau wengine kufuata mfano wao ili kuongeza nguvu katika kupambana na vifo vinavyotokana na uzazi.

Alisema kupitia ushirikiano huo wa miaka miwili, benki hiyo itatoa Sh. milioni 200 ambazo zitakazotumika kusomesha wakunga 100 katika kipindi husika na hivyo kusaidia kuongeza nguvu kazi yenye ujuzi katika kuwahudumia wajawazito.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya GF Trucks & Equipments Ltd, Mehboob Karmal, akijadiliana jambo na Kaimu Meneja wa XCMG ukanda wa Afrika kutoka China waliotembelea banda la maonyesho la kampuni hiyo, kwenye viwanja vya Biashara vya Kimataifa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango usajili watoto bila malipo wazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

WAZIRI wa Sheria na Katiba, Damas Ndumbaro, ameutaka Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) kuhakikisha mpango wa usajili wa watoto wote chini ya miaka mitano bila malipo, unatekelezwa kwa mafanikio sambamba na malengo ya Taifa ifikapo mwaka 2025.

Dk. Ndumbaro aliagiza hayo juzi kupitia hotuba yake iliyosomwa na Naibu Waziri, Pauline Gekul, wakati wa uzinduzi mpango huo kwenye Uwanja wa Mayunga. Watoto 418,246 wanatarajiwa kusajiliwa mkoani Kagera.

Aliwaomba wakazi wa mkoa huo kutumia fursa hiyo kusajili watoto wao, akisema: "Tunapenda kuona watoto wote chini ya miaka mitano wanasajiliwa chini ya mpango huu kama mlivyojielekeza ifikapo mwaka 2025. Ni matumaini ya Watanzania wote kuona mafanikio ya mpango huu."

Alisema mpango wa usajili wa watoto walio chini ya miaka mitano ni moja ya mkakati muhimu wa udhamini wa RITA kwa lengo la kuboresha hali ya usajili wa vizazi nchini.

Mbali ya kuipongeza RITA kwa hatua inazozichukua katika usajili, Dk. Ndumbaro alishukuru taasisi mbalimbali za serikali zikiwamo mamlaka za wilaya, mikoa na wadau wa maendeleo wakiwamo UNICEF, Serikali ya Canada na kampuni ya mawasiliano ya TIGO.

"Tangu mpango huu ulipozinduliwa mwaka 2015, tayari watoto milioni 8.3 wameshajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa. Haya ni mafanikio makubwa kwa RITA kwa ufanisi na kutuletea matokeo haya," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya RITA, Dk. Amina Msengwa, alisema bodi yake itaendelea kusimamia utekezaji wa maelekezo yote yaliyotolewa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa ifikapo 2030 kila Mtanzania awe amesajiliwa.

Awali Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Frank Kanyusi, alisema kutakuwa na vituo vya usajili 523 ambavyo kila kimoja kitakuwa na wasajili wasiopungua wawili waliopatiwa mafunzo maalum ya usajili na utambuzi ili kuwezesha kutimiza majukumu yao kikamilifu.

Kanyusi alisema mpango huo utatekelezwa katika awamu mbili - awamu ya kwanza itakuwa kusajili na kutoa vyeti kwa watoto ambao walikuwa hawajasajiliwa na hawana vyeti vya kuzaliwa na awamu ya pili itakuwa ni kusimika mfumo madhubuti ambao utawezesha kusajili na kutoa vyeti kwa watoto wote watakaozaliwa baada ya mpango huo kuzinduliwa.

"Mpango huo umejikita kuleta mageuzi chanya katika mfumo wa usajili wa vizazi kwa watoto kwani mpaka sasa unatekelezwa katika mikoa 23 ya Tanzania Bara na umeonyesha mafanikio makubwa, tumeweza kusajili na kuwapa vyeti vya kuzaliwa zaidi ya watoto 8,300,000," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Diaspora waombwa kuchangamkia fursa uwekezaji NSSF

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa masuala ya diaspora wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi James Bwana, amewaomba Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuona fursa ya kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) katika miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na mfuko kwenye maeneo mbalimbali nchini.

"Naomba Diaspora wote kuchangamkia miradi mbalimbali ya NSSF ikiwamo ya nyumba zilizopo Toangoma, Kijichi na Dungu jijini Dar es Salaam, pamoja na viwanja vya maeneo mbalimbali ambavyo vinauzwa kwa gharama nafuu," alisema Balozi Bwana.

Alisema hayo alipotembelea banda la NSSF na kujionea namna wafanyakazi wa NSSF wanavyowahudumia kwa weledi wanachama na wananchi wanaotembelea banda hilo.

Balozi Bwana alitoa wito kwa Diaspora wote kuitikia wito huo kwa kunufaika na fursa za uwekezaji kwa kununua nyumba na viwanja vya NSSF ambavyo ni vya uhakika.

Balozi Bwana alisema Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni mdau muhimu wa NSSF, na kwamba wanashirikiana katika masuala mbalimbali ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na NSSF zinawafikia Watanzania wote wakiwamo wanaoishi nje ya nchi 'Diaspora'.

"Natumia fursa hii kuwapongeza NSSF wamekuwa na jukumu hili kwa muda mrefu wamekuwa na mifumo mbalimbali ya kutoa huduma za Hifadhi ya Jamii kwa Diaspora, lakini hivi sasa wanakamilisha mifumo mipya ambayo itaongeza ushiriki zaidi kwa Watanzania waliopo nje ya nchi," alisema Balozi Bwana.

Alisema pia mfuko umekuwa ukiendesha miradi mbalimbali ya uwekezaji, na tayari wana ushirikiano wa karibu na NSSF na hivi karibuni wana miradi mikubwa ya uwekezaji na uendelezaji inayofanyika nchini Kenya ili kuendeleza vitega uchumi vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini nje ya nchi.

Kadhalika, uwekezaji wa NSSF hauishii katika uwekezaji wa ndani ya nchi, lakini sasa wanavuka mipaka na kwenda katika maeneo mengine nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kwenda kukusanya na kuleta faida zaidi kwa ajili kuwanufaisha wanachama wa NSSF.

"Nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, kwa kazi nzuri anayofanya ya kuhakikisha Mfuko unaendelea kusimama," alisema Balozi Bwana.

Aidha, ameipongeza Menejimenti na Bodi ya NSSF kwa kazi nzuri na miongozo ambayo wamekuwa wakiitoa katika kuhakikisha malengo makuu ya kuanzishwa kwa Mfuko yanaendelea kusimamiwa na kutekelezwa. Malengo hayo ni kuandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao.



Mkurugenzi wa Masuala ya Diaspora wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi James Bwana, akipata maelezo kutoka kwa Ofisa TEHAMA Mwandamizi wa NSSF, Rukia Haidary (kushoto), namna mwanachama anavyoweza kupata taarifa zake mbalimbali kupitia mifumo ya kidijitali ya NSSF, kulia kwa Balozi ni Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, Lulu Mengele. NSSF inashiriki Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba katika banda namba 13 la ushirikiano kati ya NSSF na PSSSF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## UDSM yaja na mradi kuzuia sumu kuvu

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kimebuni mradi wa kudhibiti sumu kuvu kwenye mazao mbalimbali ya chakula yanayohifadhiwa kwenye maghala.

Hayo yalisemwa jana na Amani Jacob wa Ndaki ya Sayansi ya Kilimo na Teknolojia ya chakula (CoAF) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wakati akizungumza na Nipashe kwenye viwanja vya Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba.

Maonesho hayo yalioanza Juni 28 yanahudhuriwa na wafanyabiashara kutoka nchi 16, kampuni 112 kutoka nje ya nchi na kampuni 1,188 za ndani.

Alisema sumu kuvu inazalishwa na fangasi anayeitwa Aspergillus flavus anayeweza kuishi kwenye joto la nyuzi 27 na kuendelea inamwezesha kuishi vizuri na kusababisha uharibifu kwenye mazao.

"Kwa mfumo wetu temperature (joto) ikifika 27 feni zitawaka kwa ajili ya kupunguza joto kwenye ghala na kwa kufanya hivyo yule fangasi hataweza kuishi mle ndani na hali hiyo itaokoa mazao dhidi ya sumu hiyo," alisema.

Alisema waliamua kuja na mradi huo kama sehemu ya kuinusuru jamii dhidi ya sumu kuvu ambayo inasababisha maradhi mbalimbali kama ya saratani ya ini.

Alisema sumu hiyo pia ni hatari na huwasababishia udumavu watoto walio chini ya miaka mitano iwapo watapewa bidhaa ambazo zina sumu ya aina hiyo.

"Kwa hiyo kwa kutumia huu mfumo wetu wa kudhibiti sumu kuvu tunatarajia tutafanikiwa kudhibiti magonjwa ya ini na mengineyo na vile vile mazao yakiwa na sumu kuvu huwa hayauziki na mwishowe wakulima watapata hasara kwa hiyo tutawakomboa wakulima," alisema.

Alisema kwa sasa hawajaanza kutumia mfumo huo kwa wakulima mmoja mmoja bali wanafanya na wakulima wanaohifadhi mazao yao kwa wingi kwenye maghala ya ushirika.

"Kwenye mradi huu tuna awamu mbili ya kwanza ni hii ila ya pili itakuja ambapo tutakwenda kwenye maghala na kuwaelezea wakulima kuhusu mfumo huu ili wauelewe unavyofanyakazi," alisema.

"Mfumo huu utawanufaisha sana wakulima kwasababu wale watakaohifadhi mazao yao kwenye maghala yenye mfumo huu mazao yao yatauzika kwa haraka sana kwasababu yatakuwa salama dhidi ya sumu kuvu," alisema.

# Utalii wa kutoa majina kuwapa faru kuanza

**Na Elizabeth Zaya**

HIFADHI ya Taifa ya Mkomazi inatarajia kuanzisha utalii utakaotoa fursa kwa watu kutoa majina ya wapendwa wao kuwapatia faru kwa ajili ya kumbukumbu ya maisha.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mhifadhi Mkuu wa hifadhi hiyo, Happinesa Kiemi, kwenye banda la Maliasili katika maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF).

Alisema watalii watakaopata fursa ya kutoa majina ya wapendwa wao kwa faru kutakuwa na gharama ya malipo na kwa watalii wa ndani ni Shilingi milioni tano na wa nje ni Dola za Marekani 5,000.

"Hii itakuwa ni moja ya utalii ambao utakuwa unaacha kumbukumbu kwa familia au ndugu wa watalii ambao majina yao yatatolewa kwa faru kwa sababu maisha yao yote watakuwa wanaitwa majina hayo, tunatarajia kuanzisha utalii huu hivi karibuni," alisema Kiemi.

"Na hata kama mtalii ambaye jina lake lilitolewa kwa faru akifariki, familia yake itakuwa inaruhusiwa kwenda kumtembelea huyo faru kwa sababu hilo jina analopewa ni la maisha na hawezi kubadilishiwa labda mpaka na yeye afariki."

Kiemi alisema badala ya watu au familia kupendelea kutoa zawadi za keki, maua fedha au mali nyingine kwa wapendwa wao ni vyema wakabadilika na kuwapatia zawadi za namna hiyo ambazo ni kumbukumbu zinazodumu.

"Tumezoea katika tamaduni zetu kwamba ukitaka kuonyesha upendo kwa mtu unayempenda unampatia maua, fedha, unamnunulia nguo na kadhalika, lakini Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi tumewaletea kitu kingine, watu waje kwetu na majina ya wapendwa wao wawapatie faru, hiyo itaongeza thamani ya namna wanavyowathamini," alisema Kiemi.

"Na tunafanya hivi ili kuwahamasisha watu hususani Watanzania, kuona umuhimu wa maliasili katika nchi yao, wenzetu wa mataifa mengine wanathamini sana vitu kama hivi, kwa hiyo tusiwaachie wafaidi wao tu na sisi kama wazawa tuchangamkie."



## Raia wa Marekani azika mabaki ya mkewe Mlima Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BALOZI wa hiari, Macon Dunnagan, raia wa Marekani, aliyekuwa akiweweseka kwa miaka 16 kutafuta namna ya kutii wosia wa mkewe aliyeagiza mabaki ya mwili wake yazikwe katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro ametimiza ndoto hiyo.

Akizungumza jana kuhusu safari yake hiyo, Macon, alisema mkewe aliyekuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa saratani ya kizazi (hakumtaja jina), mwaka 2007 aliacha ujumbe kabla ya kufariki dunia akitaka mumewe huyo kupeleka mabaki ya mwili wake katika kilele cha Mlima Kilimanjaro.

Licha ya kutii wosia huo, Macon, ameweka pia rekodi ya kuupanda Mlima Kilimanjaro na kufika kilele cha Uhuru, chenye urefu wa mita 5,895 mara 50.

Tayari, Wizara ya Maliasili na Utalii, imetambua mchango wake katika kuutangaza utalii wa Tanzania kwa kumtunuku cheti maalumu kama balozi wa hiari.

Aidha, inaelezwa kuwa uboreshaji wa miundombinu katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), uliofanywa kwa kutumia fedha za ugonjwa wa virusi vya corona na filamu ya The Royal Tour, vinatajwa kuwa sababu ya kuvutia watalii wengi kupanda mlima huo.

Kutokana na filamu hiyo iliyofanywa na Rais Samia Suluhu, inaelezwa idadi ya watalii wanaopanda mlima huo, imeongezeka kutoka watalii 12,000 mwaka 2020/2021 hadi kufikia watalii 47,000 katika mwaka unaomalizikia wa 2022/2023.

Juni mwaka 2017, pia raia wa Italia, Nico Valsesia, alipanda Mlima Kilimanjaro na kuweka rekodi ya dunia ya kuupanda kwa saa 24 hadi kileleni. Valsesia alifanikiwa kuweka rekodi hiyo ya dunia kwa kupanda na kushuka mlima huo kwa saa nane.

# Watanzania 70 hufariki kwa TB kila siku nchini

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

TANZANIA inapoteza watu 70 kila siku kutokana na ugonjwa wa kifua kikuu na kifua kikuu sugu.

Takwimu hizo zilitolewa jana na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu wakati akizungumza na makatibu wakuu na mameneja mpango wa programu za kifua kikuu kutoka mataifa 15 Afrika.

Alisema idadi hiyo inafanya wanaopoteza maisha kwa ugonjwa huo kwa mwaka kufikia watu 25,800.

"Kati ya watu 100, watu 39 waliibuliwa wakiwa wameambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu mwaka 2015 nchini Tanzania.

"Hadi sasa serikali, kupitia Wizara ya Afya, imepiga hatua katika kuibua wagonjwa wa kifua kikuu kwa asilimia 65.

Zaidi Waziri Ummy aliongeza: "Tumeongeza jitihada za kuendelea kuibua wagonjwa wa kifua kikuu kutoka mwaka 2015, ambapo katika kila wagonjwa 100 tulibua wagonjwa 39 kwa mwaka. Tumekuwa tukiwatumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii."

Kwa mujibu wa Waziri Ummy matokeo chanya katika mpango huo yametokana na uamuzi wa kuwatumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kwa sababu wao ndiyo wapo karibu na jamii.

Alisema kada hiyo ya wataalamu hupita katika vilabu vya pombe, vijiweni, nyumba kwa nyumba na kwa waganga wa tiba asili, baada ya kupatiwa mafunzo ya uelewa juu ya mgonjwa mwenye Kifua Kikuu.

Washiriki wa mkutano walijadili ni jinsi gani nchi za Afrika, zinaweza kuja na ubunifu wa pamoja na mikakati mipya ya kukabiliana na ugonjwa wa kifua kikuu.




Wakazi wa Kata ya Potwe wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakisoma majina ya wagombea udiwani kutoka vyama vya siasa baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza uchaguzi mdogo wa udiwani juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wagombea sita warejesha fomu za uteuzi udiwani

**Na Steven William,** MUHEZA

WAGOMBEA udiwani kutoka vyama sita vya siasa wamerejesha fomu zao za uteuzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi wa Kata ya Potwe, Wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Wilaya hiyo, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji, Dk. Jumaa Mhina, amethibitisha jana kuwa mpaka sasa, waliorejesha fomu hizo watoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), Sauti ya Umma (SAU), NCCR Mageuzi, Alliance Democratic Party (ADC), Chama cha Wananchi (CUF) na Demokrasia Makini.

"Nimefika katika eneo hili la uchaguzi, kwa ajili ya kukagua maandalizi ya uchaguzi huo mdogo, utakaoshirikisha wagombea wa vyama mbalimbali vya siasa. "Kiujumla, maandalizi ya uchaguzi huo mdogo wa udiwani yanakwenda vizuri. Taratibu zote za uchaguzi zimekamilika. Niwaombe wagombea kufanya kampeni za kistaarabu, kusitokee vurugu zitakazoharibu uchaguzi."

Juni 14 mwaka huu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilitangaza uchaguzi mdogo wa marudio katika kata 14 za Tanzania Bara, utakaofanyika Julai 13.


Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa NEC, Ramadhani Kailima, alisema uchaguzi huo unatokana na tume kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI), akiitaarifu kuwapo nafasi wazi katika kata 14 za Tanzania Bara.

Kata hizo zilizoko katika halmashauri 13 na mikoa tisa ya Tanzania Bara, zitakazofanya uchaguzi ni Ngoywa (Sikonge), Kalola (Uyui), Sindeni (Handeni), Potwe (Muheza), Kwashemshi (Korogwe) na Bosha (Mkinga).

Nyingine ni Mahege (Kibiti), Bunamhala (Bariadi), Njoro na Kalemawe (Same) na Mnavira (Masasi).

Zimo pia, Kinyika (Makete), Magubike (Kilosa) na Mbede (Mpimbwe) iliyoko Mkoa wa Katavi.

Ratiba ya NEC inaonyesha fomu za uteuzi, zitaanza kutolewa kuanzia Juni 24 hadi 30 na uteuzi utafanyika Juni 30, mwaka huu.



# Serikali yatenga bilioni 154/- kugharamia mbolea ya ruzuku

**Na Halima Ikunji,** TABORA

SERIKALI imesema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga Sh. bilioni 154 kwa ajili ya kugharamia mpango wa ruzuku ya mbolea ikatakayotolewa kwa wakulima, lengo likiwa ni kupunguza makali ya bei, kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uthibiti wa Mbolea Tanzania Kanda ya Kati, Dk. Stephan Ngairo, wakati akiongea na waandishi wa habari mkoani Tabora na kusema kuwa mbolea hiyo itauzwa kwa bei elekezi ili kila mkulima aweze kuimudu.

"Tayari mamlaka imetoa bei elekezi na baada ya mbolea hiyo kutolewa itaendelea kuuzwa kwa bei ileile ili tuhakikishe kila mkulima mwenye kuhitaji aweze kuipata kwa bei nzuri," alieleza.

Dk. Ngairo alisema kuwa Mamlaka ya Uthibiti wa Mbolea Tanzania imeweka mikakati ya kuvitumia vyama vya msingi ili viweze kusaidia kugawa mbolea kwa wakulima katika maeneo walipo na kueleza kuwa katika kipindi cha mwaka jana mbolea hizo ziliuzwa kwa Sh.70,000 kila mfuko mmoja.

"Niwatoe wasiwasi wakulima kwa msimu huu unaoanza kupitia maelekezo ya serikali kuanzia Julai Mosi wote mtanunua mbolea katika maeneo yenu bila ya usumbufu wowote," alisema Dk. Ngairo.

Naye Meneja Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC), Samwel Mshote, alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo imepanga kufufua shirikisho hilo ambayo imeshindwa kufanya vizuri kibiashara katika kipindi cha miaka minne iliyopita.

Alieleza kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022-2023 serikali ilitoa zaidi ya Sh. bilioni sita ili kuwezesha ushirika huo kwa ajili ya kuinua wakulima na shughuli za kilimo nchini na kwamba tayari wameingia kwenye makubaliano na vyama 20 na bado wanaendelea kuvisajili vyama vikuu ambapo chini yake kuna vyama vidogo.

Aliongeza kuwa mkoani Tabora lipo ghala lenye uwezo wa kuchukua tani 20,000 na kupitia vyama hivyo ambavyo ni mawakala wataweza kusambaza kwa haraka mbolea hiyo ili iweze kuwafikia wakulima kwa wakati.



Waziri wa Elimu, Prof. Adloph Mkenda (katikati), akitoka kufungua mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA) kwa maofisa elimu kata 2,384 kutoka mikoa yote nchini yatakayofanyika kwa siku tatu katika Chuo cha Ualimu Butimba jijini Mwanza jana. Kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, James Mdoe. **PICHA: ROSE JACOB**

# Wafamasia wapewa jukumu kulinda vifaa tiba na dawa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAFAMASIA na wataalamu wa maabara kutoka Kanda ya Kagera wamepewa jukumu la kulinda na kutunza vifaa tiba pamoja na dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Pia wametakiwa kuhakikisha bidhaa hizo hazikosi katika maeneo husika kwa mstakabari wa maisha ya wananchi.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mkoa wa Geita, Dk. Omary Sukari, wakati wa kikao cha majadiliano cha hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya kwa Kanda ya Kagera inayojumuisha wilaya ya saba za mkoa huo na wilaya tatu za Mkoa wa Geita.

Dk.Sukari alisema mchakato wa upatikanaji wa bidhaa hizo unaanzia kwa wataalamu kwa kuanza kufanya makadirio kila unapoanza mwaka wa fedha serikalini, kwamba kukosekana kwa vifaa hivyo ni uzembe wa wataalamu hao.

Alisema kuna kila hali ya kuangalia bidhaa gani ipo kwa kiwango cha kutosheleza au iko chini na wingi upi haitumiki na kutojulikana matumizi yake na kufanya dawa kuisha muda.

"Ngazi ya vituo ifanye hiyo na kote hadi mkoa kwenda wizarani hadi kufikia kupelekwa kwa wenzetu wa Bohari Kuu ya Dawa ambao wanapelekewa oda zinazotakiwa katika ngazi husika ili dawa ziletwe," alisema Dk. Sukari.

Aidha, alisema kituo kikiwa na bidhaa hufanya mteja akitoka kwenye huduma afarijike kulingana na huduma aliyopata kupitia vifaa tiba, lakini manung'uniko yanaanzia pale mteja anapokosa kile anachohitaji na serikali haiwezi kujua uhitaji wa kituo husika bila taarifa kutoka kwa wataalamu waliowekwa katika eneo husika.

Meneja wa MSD Kanda ya Kagera, Kalendero Masatu, alisema yapo mategemeo ya kuwa na ongezeko la upatikanaji wa dawa kwa asilimia 70 hadi 80 na kueleza kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita ongezeko la dawa lilikuwa 65.

Aliongeza kuwa ongezeko hilo lilifanya kuwa na asilimia 90 ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya ambazo hufanya oda na (MSD) watoa huduma ambao ni wafamasia na wataalamu wa maabara.

Alisema: "Na jambo hilo hufanya kuleta mnyororo wa ugavi ulio bora katika utoaji wa vifaa tiba kwenye vituo vya afya na oda zinatolewa kulingana na uhitaji wa mteja katika kituo chake ambacho anafahamu kulingana na makadirio na kusaidia ili dawa zikiletwa zisiishe muda wake kabla hazijatumika."

# Babu adaiwa kumrubuni mwanafunzi, ampa ujauzito

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamsaka Amos Samsoni (65) Mkazi wa Kijiji cha Mwamala Kata ya Kolandoto Manispaa ya Shinyanga, ambaye amekimbia kusikojulikana akituhumiwa kumpatia ujauzito mwanafunzi wa kidato cha kwanza (16) katika Shule ya Sekondari Kolandoto (jina limehifadhiwa).

Akitoa ufafanuzi juu ya tukio hilo juzi, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Janeth Magomi, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kusema kuwa mzee huyo ambaye kwa sasa ametokomea kusikojulikana wanaendelea kumsaka ili achukuliwe hatua za kisheria.

"Jeshi la Polisi tunamtafuta mtuhumiwa ambaye amedaiwa kumpatia ujauzito mwanafunzi sababu alitoroka kabla hajakamatwa," alisema Magomi.

Mwanafunzi huyo akielezea namna alivyoingia kwenye mahusiano ya kimapenzi na mzee huyo, alisema alimuita nyumbani kwake na kumpatia Sh. 2,000 na siku nyingine alimpatia Sh.5,000 kisha akamlazimisha kufanya naye mapenzi.

Alisema baada ya hapo waliendelea kuwa wapenzi hadi akashika ujauzito, lakini baadaye alichukizwa na kitendo cha mzee huyo kumtaka tena ndugu yake kimapenzi.

Alisema hali hiyo ilimlazimu kwenda kutoa taarifa katika familia kuwa amepewa ujauzito na mzee huyo ambaye ni Katibu wa Kijiji.

Aidha, alisema baada ya kikao cha familia kukaa kujadili jambo hilo, walikubaliana mzee huyo atoe faini ya magunia mawili ya mpunga na baiskeli ili kumaliza suala hilo, huku yeye akiacha masomo na kubaki kulea ujauzito ambao kwa sasa una miezi mitano.

Baada ya kikao hicho cha familia, baadhi ya wanawake katika kijiji hicho hawakukubaliana na jambo hilo wakidai mzee huyo amekuwa na tabia ya kurubuni wanafunzi na kufanya nao mapenzi na kuwaharibia maisha yao, ndipo wakatoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ili akamatwe.

Nao wadau wa kupinga vitendo vya ukatili mkoani Shinyanga wakiwamo (SMAUJATA), wameliomba Jeshi la Polisi mkoani humo kuhakikisha wanamkamata mzee huyo na kuchukuliwa hatua kali za kisheria ili liwe fundisho kwa watu wengine.

ama
ALHAMISI JULAI 6, 2023
AFYA NA MAZINGIRA




## Huu ndio ugonjwa sonona, Hospitali Sekou- Toure inavyopambana nao

Ukurasa 12



## MTAALAMU WA VETA
## Mbaazi, zao linalochuana na ngano kwa mambo mengi, lishe ikiwa juu

Ukurasa 14

# Agizo la Samia; Pwani bila kuni, mkaa, operesheni imepamba moto

- Ni angalizo alilotoa kuhamia gesi
- Makamba aanika ilikofika wizara

**Na Khadija Kalili, Kibaha**

KITAIFA, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na serikali yake wako katika kampeni ya kutunza mazingira inayojumuisha kuondokana na utumiaji kuni na mkaa katika shughuli za jikoni.

Mnamo Novemba mwaka jana, Rais akaelekeza kuundwa kikundi kazi cha kupitia na kuchakata sera zilizopo, kuelekea kwenye mpango wa taifa kuondokana na matumizi ya gesi chafu kupikia, ifikapo mwaka 2032.

Ni maelekezo aliyoyatoa katika ufunguzi wa mjadala kitaifa kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Kikundi kiliochoundwa kinaongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Nishati, ikiratibu na kufanya shughuli za sekretarieti za kikundi hicho.

Ili kufikia tija na ufanisi, Rais Dk. Samia akaagiza kikundi kijumuishe wataalamu kutoka idara na taasisi za umma, sekta binafsi na wadau wa mazingira.

"Kikundi kazi kikapitie sera na miongozo mbalimbali, ili kije na mpango mkakati na dira ya miaka 10, kikielekeza mambo muhimu ya kufanya ili ifikapo 2032, kila mtu atumie nishati safi ya kupikia," anatamka Rais Dk. Samia.

Kama ilivyo kawaida yake kuwatetea kinamama, akasema matumizi ya nishati safi kupikia yatawasaidia wanawake kuondokana na adha ya kutafuta kuni porini, wakiwa hatarini kukabiliwa na wanyama wakali, hata nyoka.

Pia akataja muda wanaoupoteza porini kutafuta kuni, sasa utumike kuzalishaji mali ikiwamo ufumaji na biashara, akiahidi mkakati wa kibajeti katika muda mfupi ujao ni kuanzishwa mfuko wa nishati safi ya kupikia, utakaotafiti, kuwekeza na kutatua changamoto.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Dk. Selemani Jafo, akihamasisha wakazi kuacha kutumia kuni na kujikita kwenye gesi, katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ruvu, wilayani Kibaha mkoaani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Nishati, ikamnukuu Dk. Samia, kwamba, takwimu zinaonyesha kaya zinazotumia gesi nchini kupikia ni asilimia tano pekee, huku watumiaji umeme ni asilimia tatu.

Vilevile taarifa hiyo inamrejea Daktari Paulina Chale, kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, kwamba wagonjwa wa mfumo wa hewa ni wengi, yakiwamo yanayosababishwa na kutumia kuni na mkaa kwa muda mrefu.

Waziri wa Nishati, January Makamba, katika kupokea agizo hilo, akaahidi kusimamia na utekelezaji wa maagizo yote hayo ya rais, katika safari ya kuelekea lengo la serikali ifikapo mwaka 2032.

**WAZIRI MAKAMBA**

Ikiwa sehemu ya utekelezaji agizo la Rais miezi minne kabla, Waziri Makamba mnamo Machi mwaka huu, akaahidi ndani ya miezi mitatu ingezinduliwa Dira ya Taifa Kuhamia Matumizi ya Nishati Safi ya Kupika, pia Mpango Mkakati wa Utekelezaji Dira hiyo.

Akadokezea angalizo kuwa serikali ingechukua hatua kuwezesha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia, ifikapo mwaka 2033.

"Takwimu zinaonyesha asilimia nane tu ya Watanzania ndio wanatumia nishati safi ya kupikia (fesi na umeme), hivyo Mheshimiwa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan ameshatoa maelekezo kuwa ndani ya miaka 10 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia, ameshatuelekeza tutengeneze Dira, Mkakati na Mweleko..." anasema.

Makamba anafafanua, mfuko utaweka ruzuku itakayowawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei ya gesi,: akihitimisha"...kazi kubwa, lakini inawezekana na 'Kazi Inaendelea'..."

Anaeleza kuwa serikali ya awamu ya sita imeamua kulivalia njuga suala la nishati safi, ikiwa ni katika jitihada zake za kuboresha maisha ya Watanzania, hasa kinamama.

Makamba anawarejea wasomi wa afya akitamka: "Wataalamu wanasema, saa moja jikoni ni sawa na sigara 300. Sasa hapa unategemea ustawi utatoka wapi? Bahati nzuri Mheshimiwa Rais, ameliona...."

**PWANI YATEKELEZA**

Ikiwa sehemu ya kuungana na Wizara ya Nishati, mkoa wa Pwani ukaandaa kongamano la siku mbili kujadili hoja ya kitaifa ya Nishati Safi ya Kupikia, ikiwa ni maelekezo na Dira ya Rais Dk. Samia, kuhamasisha matumizi ya nishati safi kupikia.

Ni mjumuiko wa washiriki 200 waliopatiwa mitungi ya gesi, ikiwa sehemu ya uhamasishaji nishati safi kupikia, wakiacha kuni na pia mkaa.

Mamalishe, wajasiriamali na wananchi kwa ujumla kutoka mikoa ya Dar es es Salaam na Pwani waliohudhuria, wamewapongeza waandaaji, Jumuiya ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TABWA), wakiongozwa na mkuu wao, Noreen Mawalla.

Anakiri kutambua juhudi za serikali ya awamu ya sita kumtetea mwanamke dhidi ya changamoto hizo za kiafya, mazingira na ustawi unaomkabili kutokana na kutumia kuni na mkaa

"TABWA tumefurahishwa na mwitikio mkubwa wa wafanyabiashara waliojitokeza katika kon-

Inaendelea Uk. 14

AFYA

# Huu ndio ugonjwa sonona, Hospitali Sekou- Toure inavyopambana nao

## • Daktari Bingwa: Wengi wanaoniona wana shida hiyo

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

MIONGONI mwa magonjwa ya matatizo ya afya ya akill, imo sonona. Mtaalamu wa afya ya magonjwa ya akili kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza -Sekou-Toure, Dk. Meshack Samwel anasema unaweza kusababishwa na msongo wa mawazo kwa binadamu kwa muda mrefu.

Anasema mara nyingi unakuwa zao la mfadhaiko wa akili, mtu anashindwa kujua anachokifanya au anachotakiwa kufanya na hajui kutatua jambo linalomkabili mbele yake, shida tabu au matatizo.

Mtaalamu huyo anaeleza kwamba chanzo chake kikuu ni msongo wa mawazo wa muda mrefu, unapomsababishia mtu kupata shida hiyo. Anataja dalili zake ni kwa mgonjwa muda wote anapoteza matumaini ya maisha yake, hana ari ya kufanya kazi, pia anakata tamaa kimaisha.

Dk.Samwel, pia anaeleza sababu ni kwa mhusika anakuwa amerundika vitu vingi kichwani bila ya kupata ufumbuzi.

Msongo wa mawazo wa muda mrefu unatajwa nao unaweza kumsababishia mtu kupata ugonjwa huo wa sonona, hali inayoweza kufikia hatua mtu anachanganyikiwa akili, anasahau mambo kila wakati na anakosa amani akiwa mwenye huzuni maishani mwake.



Dk. Meshack Samwel, mtaalamu wa afya ya akili katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa, Sekou Toure, Mwanza. **PICHA: MTANDAO**

Mtaalamu huyo anataja zao lake ni mtu anachukua hatua mbaya kama ya kujiua kupitia matendo au matukio kama ya kujinyonga, kujirusha kutoka ghorofani au anavuka barabara koholea au kwa makusudi, anaishia kugongwa na gari.

Hata hivyo katika maelezo yake, Dk. Samwel anatahadharisha kuwapo tofauti ya msongo wa mawazo na sonona, kwamba ni vitu viwili tofauti, ingawa zina vyanzo vinavyofanana.

Katika msongo wa mawazo, mtu anasongwa na mengi, ila anakuwa hajavipatia ufumbuzi, hivyo vinamsababishia magumu kama kupata shinikizo la damu, kukosa mahitaji ya kifamilia, au kufiwa na mtu wa karibu.

Dk. Samwel anasema robo ya watu walioenda kupata huduma katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza -Sekou -Toure, wanakabiliwa na sonona, kwa wastani kila wanne wanaoenda hapo kupata huduma ya aina hiyo, mmoja hukutwa na dalili za ugonjwa huo, unaosababishwa na msongo wa mawazo.

Inakadiriwa wanaojiua kutokana na sonona kila siku, idadi yao inafika 800,000. Pia katika utafiti wa nchini, mwaka 2019 kulionekana asilimia nne hadi tano ya watu wanajiua kutokana na ugonjwa huo, huku kukiwapo magonjwa mengine ya afya ya akili yanayohusishwa na imani za kishirikina.

Wataalamu wa afya katika Hospitali ya Sekou -Toure, wanasema wako mstari wa mbele kutoa huduma kwa wagonjwa wake, elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari, mikutano ya hadhara ya wananchi, semina na kongamano za kijamii.

Vilevile, katika sura ya pili wanajitambulisha kuwa ni watoaji ushuari maarufu katika jinsi ya kukabiliana na hali ya ugonjwa huo, kutoa dawa za matibabu na ushauri wa kisaikolojia inayojumuisha eneo la msongo wa mawazo, ili kusaidia kuwarudisha katika hali zao za kawaida.

Tiba ya awali ya fya ya akili, ni hitaji la utulivu mkubwa, kwa sababu magonjwa mengine yana asili ya usugu, hata kuwa rahisi kujirudia kila mara.

Inatajwa watu wenye umri kuanzia miaka 24 hadi 45 ndiyo wanaotajwa zaidi kukabiliwa na ugonjwa huo, hasa wasio na elimu, ajira kuvunjika ndoa, masikini zaidi sawa wako katika jumla ya asilimia 46 hadi 50.

Vilevile suala la upweke, uzee, ugane na ujane linatajwa katika kundi la watu wanaostahili kusaidiwa kisaikolojia na wataalamu wa afya, kwa sababu ni janga linaloendelea kuitesa dunia, ikihitaji kupatiwa ufumbuzi.




# AGIZO LA SAMIA; PWANI BILA KUNI, MKAA, OPERESHENI IMEPAMBA MOTO

**Inatoka Uk. 11**

gamano letu na tumewasikia walivyokuwa wanaelezea umuhimu wa kutumia nishati safi ya kupikia, wakiwa wamesikiliza mada na kupata nafasi ya kuuliza maswali na kujibiwa," anatamka.

Mawella anasema, wengi wameahidi kuwa mabalozi wakubwa katika jamii wanakotoka, hasa kwenye kutoa elimu ya umuhimu wa matumizi ya Nishati Safi," anasema Mawalla, huku akifafanua wamewahusisha zaidi wanawake, vijana, wauza mkaa, watengenezaji na wauzaji majiko ya nishati safi.

Aidha, anasema baada ya kutoa elimu kwa wanawake wa Dar es Salaam na Pwani, anaahidi kongamano kama hilo litafanyika kwenye mikoa ya Mtwara, Lindi, Morogoro, Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa.

"Tumepanga kutoa elimu, kupanga mikakati ya utekelezaji na kujenga mtandao wa biashara kwa ujumla katika mikoa mbalimbali kama sehemu ya kumsapoti Mama Samia Suluhu," anasema Mawalla.

**JAFO AWAPONGEZA**

Mnamo Aprili 19, mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, ambaye ni Mbunge wa Kisarawe, ameupongeza mkoa atokao wa Pwani, kwa kuwa na kampeni ya upandaji miti, ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Ni kauli yake kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ruvu, iliyopo Mlandizi, Kibaha Vijijini wakati wa kuzindua Kampeni ya Utunzaji Mazingira na Matumizi ya Nishati Mbadala kwa mkoa huo, ikishirikisha Benki ya NMB, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) mkoa Pwani, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kampuni ya Taifa Gas.

Waziri Jafo anasema, ni kampeni ikatayosaidia kutunza mazingira na kutangaza teknolojia mbadala ya matumizi ya nishati, kwa kupunguza matumizi ya miti kama nishati kwa ajili ya kupikia na matumizi mengine ya binadamu ya kila siku.

Anaitaja Pwani kuwa katika orodha ya mikoa minne iliyoathirika sana na uharibifu wa mazingira na baada ya kupata maelekezo ya Rais Dk. Samia, kuhusu marekebisho ya mazingira yake, mkoa umejiongeza kwa kubuni kampeni za kujikwamua na athari za kimazingira.

Waziri Dk. Jafo, katika halfa hiyo akazindua mtambo mkubwa wa gesi shuleni hapo wa kutumika kwenye jiko la shule, kuhakikisha wanaachana na matumizi ya kuni na mkaa hapo.

Pia, akashauri kampuni zinazozalisha nishati safi kufanya mazungumzo na taasisi za kiserikali, hospitali, shule na kambi zote za kijeshi, wafikie makubaliano kuwawezesha kufunga mitambo ya gesi kwa malipo ya awamu, waachane na mkaa, pia kuni.

**RC KIBAHA**

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Alhaji Abubakari Kunenge, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson John, anasema mkoa wao umeweka mikakati ya kutunza mazingira, ikiwamo kupanda miti milioni 13.5.

Anasema, hadi sasa wameshapanda miti milioni 9.7, ikiwa ni zaidi ya asilimia 85 ya malengo waliojiwekea kurejesha uoto wa asili uliokuwapo awali, kabla ya uharibifu uliotokea.

Dk. Jafo anasema mkoa umejipanga kuwaondoa vijana waliojiajiri kwenye biashara ya kukata miti na kuchoma mkaa, wanakusanywa kupewa ajira mbadala kwenye viwanda vinavyotarajiwa kuanzishwa vya nishati mbadala.

Mkurugenzi wa kampuni ya Taifa Gas, Anjela Bhoke, anasema kila mwaka kuna ekari 400,000 za miti nchini zinapotea kutokana na matumizi nishati ya miti, hivyo mchango wao unajumuisha mikakati ya kujenga kiwanda cha kutengeneza mitungi ya gesi, wakilenga kuisambaza majumbani na kwenye taasisi za umma.

Mwakilishi wa Benki ya NMB, Seka Urio, anasema kuwa wametenga shilingi milioni 470 mkoani Pwani, kuhamasisha shule zitakazopanda miti 2,000 na kuitunza kwa asilimia 80 kila moja itapatiwa shilingi milioni 50; mshindi wa pili miti 1,500 akipata shilingi milioni 30 akiitunza kwa asilimia 70; wa tatu atazawadiwa shilingi milioni 20 kwa kupanda miti 1,000 itakayotunzwa kwa asilimia 70.

MAZINGIRA

## KAMATI MAALUM KAZINI

# Zijue harakati za kunusuru binadamu na wanyama kupitia shoroba salama

**Na Salome Kitomari**

SEHEMU ya changamoto kubwa inayowakabili wanyamapori, ni kupungua njia za kuunganisha eneo lililohifadhiwa, kwenda jingine, au maeneo ya mtawanyiko maarufu kama shoroba, ambazo nyingi zimevamiwa na shughuli za kibinadamu.

Hadi sasa Tanzania ina shoroba 61 zinazounganisha hifadhi za taifa, mapori ya akiba, pia mapori tengefu, ili kukamilisha ikolojia, hali inayotajwa kuleta ulazima kwa wanyamapori kuhame kutoka eneo moja kwenda jingine kufuata malisho.

Ni mwendo unaojumuisha kufuata madini muhimu au kuchanganya uzazi, kuepusha kuzaliana ugonjwa, maana vinginevyo watateketea, hata kuwapoteza.

Mwaka 2009, Mamlaka ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), ilifanya utafiti na kubaini bila hatua za makusudi ifikapo mwaka 2050, Tanzania itabakiwa na Hifadhi ya Taifa Ruaha na Pori la Akiba Selous, zingine zinazobakia zitakuwa na umri wa kuhesabu.

Shoroba 20 zina mpango wa kitaifa kuzinusuru, ili kuwezesha wanyama kutembea eneo moja kwenda jingine na kufanikisha hilo kuna hatua zimechukuliwa.

Wahusika, Taasisi ya Kusimamia Uhifadhi wa Tembo wa Kusini (STEP) kwa ufadhili wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, wameshaongoza Shoroba ya Tembo ya Kilombero, kitaalamu inaitwa Nyerere-Selous -Udzungwa.

Wataalamu wanatahadharisha, iwapo hatua za uokoaji zisipochukuliwa ndani ya miaka mitano, hazina tajwa zitapotea na ndiyo maana wameanza na Shoroba ya Nyerere-Selous-Udzungwa, itayowekewa uzio wa umeme na njia ya kupita wanyama chini ya barabara kuu ya Mikumi-Kilombero-Ifakara.

### DARAJA LA CHINI

Meneja wa Shoroba wa Taasisi ya STEP, Joseph Mwalugelo, anasema lengo kuu la kuanzishwa hifadhi ya Tembo Kusini mwa Tanzania, ni imani katika ustawi wa jamii karibu na mipaka ya hifadhi na ulinzi bora wa maliasili hususan tembo, kwa kushirikiana na wadau jirani.

Anaeleza tembo wanapotoka eneo moja lililohifadhiwa kwenda jingine, huwa anafanya uharibifu wa mazao kutokana na uzito wake; tembo mkubwa ana tani saba na mtoto kilo 500.

Mwalugelo anasema shoroba hiyo itapita katika Kijiji cha Kanyenja, chenye ukubwa wa kilomita za mraba 23.5 na zilizochukuliwa ni kilomita 1.2 sawa na asilimia tano.



Mwonekano wa shoroba ya tembo Kilombero, kando ya mashamba ya miwa na eneo lililofyekwa na sasa limelipwa kupisha maboresho ya shoroba. **PICHA: SALOME KITOMARI**

Katika Kijiji cha Mang'ula, zimechukuliwa mita za mraba 600 kati ya kilomita 5.1, sawa na asilimia 11 ya eneo, huku kijiji cha Sole wakichukua kilomita za mraba 0.28 (mita za mraba 280), kilomita 3.8 sawa na asilimia saba, kufanya jumla ya urefu wa shoroba hiyo kuwa kilomita 12.5, ikiwa na upana kati ya mita 150 hadi 200.

"STEP ilianza kwa kuzuia wanyama waharibifu kwenye mashamba kwa kutumia mbinu mbalimbali, awali jamii ilitukataa kabisa ikidhani tunakwenda kuwanyang'anya maeneo yao ili yawe hifadhi, lakini taratibu walituelewa hadi wakakubali kutoa eneo ambalo tumelipa fidia," anasema.

Anasema, baadhi ya wanavijiji na viongozi walipelekwa nchini Kenya kuona daraja la chini lililojengwa na kuwekewa uzio wa umeme kwa wanyama kama tembo ikiwadhibiti upitaji wao kutoka eneo moja lililohifadhiwa kwenda jingine, huku wananchi jirani wakiendelea na shughuli zao, vilevile wakinufaika na utalii.

Mwalugelo anasema, utafiti umebaini zaidi ya makundi 26 ya tembo yenye wastani wa tembo 10 kila moja, hupita kwenye eneo hilo na kamera ina makundi 12 eneo la Nyerere na sita Udzungwa, akinena uongozi wa wilaya umeunda kamati yake ya shoroba.

Mratibu huyo anasema, zaidi ya hekta 219 zimethaminishwa na Sh. bilioni mbili zimelipwa kwa wananchi wa Kanyenja, Sole na Mang'ula 'A', Tarafa ya Mang'ula.

Anasema pamoja na fidia, kila kijiji hupata fedha ya kuhudumia kijamii kadri ya vipaumbele vilivyopo, vikiwapo vikundi vya ujasiriamali na mikopo, lengo ni kuimilikisha jamii kuona tembo wenye maisha.

"Tunapotoa msaada wowote kwa jamii, hata kabla hawajakubali mradi tulikuwa tunasema 'tembo amewafadhili' tulitaka waone thamani ya kutunza tembo na sasa wamekuwa mabalozi wazuri na shoroba inafunguka.

"Yapo maeneo walikuwa hawalimi kabisa ila sasa kwa misimu miwili wamelima na kuvuna kutokana na mbinu za kuzuia na kufukuza tembo tulizowafundisha, tunaamini baada ya mradi kukamilika wananchi wataishi kwa amani zaidi," anasema Mwalugelo.

### USAID NA MALIASILI

Mratibu wa Sera na Utafiti wa Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, Olila Joseph, anasema wanashirikiana na STEP, pia serikali katika kuongoa shoroba za wanyamapori nchini na wamechagua saba zilizo katika hali mbaya.

"Tulivyoanza kulikuwa na migogoro mingi na mikubwa baina ya tembo na binadamu, lakini sasa wananchi wameelewa na kumudu mazingira ya tembo, sasa tunasaidia ujenzi wa shoroba ya kisasa ambayo ni ya kwanza Tanzania.

"Tulianza 2018 kwa Mradi wa Protect hali haikuwa nzuri na tunaona mwelekeo mzuri na wamekubali kutenga maeneo ya kuruhusu tembo kupita salama kwenda eneo la misitu, Hifadhi ya Taifa Nyerere na Pori la Akiba Selous," anasema.

Anafafanua kila mradi unaotekelezwa na USAID wanajitahidi uwe endelevu kwa kuhusisha serikali na wananchi tangu unapoanza na ndiyo maana wameshiriki kuhakikisha kunakuwapo Kamati ya Taifa ya Kuongoza Shoroba na Ngazi ya Wilaya, kukiwapo kamati ya shoroba.

Olila, ambaye ni Mratibu wa Mradi wa Tembo wa Kilombero, anasema wataendelea na wadau wengine kuzifikia shoroba zote 61, serikali ikiweka msisitizo kwenye hizo 20, zisipotee ndani ya miaka mitano ijayo.

Anazitaja shoroba wanazozihudumia ni: Kwakuchinja inayounganisha Hifadhi ya Taifa Tarangire na Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara; Nyerere-Selous -Udzungwa; Amani Nilo; Mahale-Katavi; Burigi Chato-Kigosi -Moyowosi' Ruaha-Rungwe Inyonga na Ruaha-Rungwa.

"Kila shoroba ina changamoto tofauti na ina utaratibu tofauti wa kuongoa. Hii (Kilombero) iko karibu sana na mashamba na makazi ya watu, ndiyo maana tumeona umuhimu wa kuweka fensi ya umeme, ila kuna nyingine ni kubwa, pana na maeneo ya wazi mfano Kwakuchinja mkoani Arusha huwezi kuweka fensi," anasema.

Mratibu huyo anasifu Chama cha Waandishi Habari za Mazingira Tanzania (JET), kimekuwa na mchango mkubwa katika uhifadhi, hususani uongozaji shoroba, kwa kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari.

### KAMATI KITAIFA

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kuongoa Shoroba, Lina Kitosi, anasema kamati inajumuisha wataalamu wa Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zake za Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA), Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara ya Maji na Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

"Shoroba ya Nyerere-Selous - Udzungwa ni kati ya 61 za kitaifa zinazopaswa kutambuliwa na wananchi na kuzingatia maelekezo ya serikali, kwa kuepusha kufanya shughuli za kibinadamu kwenye mapito ya tembo. Tuna mpango kazi wa kitaifa wa miaka mitano ambao ni lazima utekelezwe na kila mamlaka," anasema.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Wanyamapori Tanzania, Dk. Fortunata Msofe, anakumbusha lengo la kuongoa shoroba ni kupunguza matukio ya wanyama wakali na waharibifu na baada ya kuziainisha na kuwekea uzio unaofaa, wanyama watapita kwenye maeneo yao na binadamu ataendelea na shughuli zake kama kawaida.

"Hali ya shoroba nchini siyo nzuri kutokana na ongezeko la watu na shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya shoroba 61, ndiyo maana tumeainisha 20 ambazo tusipochukua hatua zinapotea ndani ya miaka mitano," anasema na kuongeza:

"Ni utekelezaji wa kanuni za mwaka 2028 za Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009, zinaainisha kwamba jukumu la kuainisha na kuwekea alama za kudumu ili wananchi waelewe maeneo fulani ni hatarishi kwa makazi na kilimo, linatakiwa kufanywa na wizara ambayo inashirikisha taasisi nyingine na wadau wa maendeleo."

Anasema, serikali inasisitiza kuwapo mpango wa matumizi bora ya ardhi, ili wananchi waelewe matumizi ya kila kipande cha ardhi na tayari serikali imeshaainisha shoroba ambazo watu wakiendelea kuishi watadhurika.

### SHOROBA ZENYE HATARI

Msofe anazitaja shoroba za kipaumbele zilizo hatarini ni: Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) na Hifadhi ya Taifa Serengeti, eneo la Yaeda Chini, Nyerere-Selous-Udzungwa, Kwakuchinja, unaounganisha Hifadhi ya Taifa Ruaha na Rugwa na Kitulo, unaounganisha Tanzania na Msumbiji unaojulikana kama Selous -Nyasa.

Nicolaus Kasangara, mkazi wa Kijiji cha Mang'ula, wilayani Kilombero, mkoa wa Morogoro, anasema kutengenezwa shoroba hiyo kutapunguza kero ya tembo wanaoharibu mazao, pia wananchi kuuawa.

"Tumeteseka kwa muda mrefu, sasa tumepata suluhisho ile hali ya tembo kuzagaa mtaani, kuharibu na kula mazao yetu itakuwa historia. Lakini, tunatarajia ongezeko la watalii ambao wataona namna wanyama wanavuka kutoka Hifadhi ya Taifa Udzungwa kwenda Hifadhi ya Taifa Nyerere na Pori la Akiba Selous," anasema.

AFYA

## MTAALAMU WA VETA

# Mbaazi, zao linalochuana na ngano kwa mambo mengi, lishe ikiwa juu



Sehemu ya mlo wa mbaazi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Pilly Kigome**

KUNA waliokariri kwamba zao la ngano ndio linaloweza kutumika katika mapishi mbalimbali ya aina tofauti, hata kuwapo watu wameipa sifa kuu ikiwa na ishara haina mpinzani wa kufanana nayo kwa 'mambo mengi.'

Watu hao wamekuwa wakiipatia wasifu katika staili ya lugha wanayoambiana "una mambo mengi kama unga wa ngano."

Hilo limefikia hatua hata kuwapo baadhi ya watu kuiona kwa upekee wake, wengi wakiamini hakuna zao linaloipiku, kumbe ukweli wake unaakisi ni zao la kukosekana uelewa sahihi katika ngazi hiyo.



> Pili, mtaalamu Mwaikuju anataja kwamba watu wengi aina ya mapishi mbalimbali ya zao hilo, huku baadhi zaidi ya wazalishaji wanalichukulia kuwa zao la biashara inayosafirishwa nje ya nchi, wakajipatie fedha.

Lipo zao la mbaazi linalochuana na ngano. Hilo linaangukia katika mmea jamii ya kunde unaokuzwa sana katika ukanda wa tropiki duniani, huku nchini Tanzania kukiwapo hisa kubwa ya uzalishaji na baadhi ya wakazi kunakozalishwa wanaipa sifa ni za la asili.

Nchini zao hilo linalolimwa zaidi katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Kusini na Kanda ya Kati.

Mtaalamu na Mwalimu Mwandamizi wa Vyakula na Vinywaji, katika Stadi za Hoteli na Utalii, kutoka Chuo cha Ufundi (VETA), Robinson Mwaikuju, anaiambia Nipashe kuwa mbaazi ni maarufu sana katika jamii, hasa ile ya mikoa ya Pwani na hutumika kama chakula katika nafasi hasa ya mboga.

Hata hivyo, anakosoa kwamba bado sehemu kubwa ya jamii kwa ujumla, imekosa uelewa wa kutosha kuhusu zao hilo na mengi yanayoambatana nayo, kwa kuwa watu wengi wamekuwa hawali mbaazi kwa wingi.

Anasema, utafiti unaonyesha kwamba watu wengi hawali mbaazi, kutokana na sababu tofauti, ikiwamo kukosa inayohusu zao na mlo huo, pia faida zake katika nafasi yake katika lishe.

Pili, mtaalamu Mwaikuju anataja kwamba watu wengi aina ya mapishi mbalimbali ya zao hilo, huku baadhi zaidi ya wazalishaji wanalichukulia kuwa zao la biashara inayosafirishwa nje ya nchi, wakajipatie fedha.

Mtaalamu huyo anasema chakula mbaazi kina matumizi na faida nyingi za kiafya, ikiwamo kuna wakati inasagwa kuwa katika mfumo wa unga.

Mwaikuju anadadavua faida za kiafya kutoka kwenye mbaazi, kwamba ina madini muhimu aina ya chuma na zinki pamoja na kalsiamu ambazo ni muhimu kwa afya ya mwanadamu.

Vilevile, inatajwa niu mlo wenye virutubisho vingi vinvyojumuisha protini na vitamini B.

> Lipo zao la mbaazi linalochuana na ngano. Hilo linaangukia katika mmea jamii ya kunde unaokuzwa sana katika ukanda wa tropiki duniani, huku nchini Tanzania kukiwapo hisa kubwa ya uzalishaji na baadhi ya wakazi kunakozalishwa wanaipa sifa ni za la asili.

**FAIDA KIUCHUMI**

Kiuchumi, Mwaikuju anaainisha faida lukuki za kiuchumi zitokanazo na mbaazi ikiwamo kurutubisha ardhi hivyo inapunguzia mkulima gharama za kilimo, kwani haina ulazima kupanda na mbolea.

Faida ya pili kiuchumi analitaja zao hilo ni chanzo cha ajira kwa wanaofanya kazi katika mnyororo wake wa thamani, zao mbaazi linapozalishwa.

Vilevile anaainisha manufaa mengine ya kutumika kama chakula cha mifugo, huku zao hilo linabaki kuwa nishati ya kupikia na wakati huohuo, inaiongezea familia kipato.

Lingine kwa mujibu wa mtaalamu Mwaikuju, linastahimili ukame, hapo akiorodhesha vyakula vitokanavyo na unga wa mbaazi, baadhi ni; skonzi, chapati za maji, chapati za kusukuma, sambusa, kababu, mkate, keki, mandazi, donate na hafu keki.

Pia, anataja supu, futari, ndizi za mbaazi, kande, rojo na biriyani ya na mbaazi .





## JKT yahimiza wazazi kupeleka watoto kliniki

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

MKURUGENZI wa Ustawi wa Jamii wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kanali Regina Matina amewataka wazazi kujenga utaratibu wa kupeleka watoto kliniki kwa ajili ya kupata chanjo ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Mbali na hilo ameshauri jamii kuzingatia suala la utunzaji mazingira kwa kujiepusha na kutupa taka ovyo.

Kanali Matina alitoa kauli hiyo jana katika Hospitali ya Halmashauri ya Chamwino walipokuwa wakifanya usafi kwenye hospitali hiyo sambamba na utoaji zawadi ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo tangu lianzishwe.

Alisema kuna umuhimu mkubwa wa jamii kutambua huduma za matibabu anazotakiwa kupata mtoto katika ukuaji wake, hivyo ni vema jamii ikazingatia suala la mahudhurio ya kliniki za watoto kwa muda unaotakiwa.

"Ni vizuri jamii ikazingatia makuzi na malezi ya mtoto na moja ya vitu vya kuzingatia ni kumpeleka kliniki mtoto ambako huko utapata elimu ya lishe bora kwa mtoto kutoka kwa wataalamu wa afya," alisema Kanali Matina.

Akizungumzia kuhusu ziara hiyo pamoja na kitendo cha kufanya usafi katika hospitali hiyo, alisema ni sehemu ya maadhimisho ya 60 ya JKT toka lianzishwe lakini pia pamoja na kuunga mkono jitihada za serikali za kutunza mazingira kwenye kila eneo husika.

Alisema kila siku serikali inasisitiza utunzaji wa mazingira ndiyo maana nao wameamua kufanya usafi katika hospitali hilo ili kuzidi kuweka safi mazingira ya eneo hilo.

Zawadi walizotoa katika hospitali hiyo kwa wagonjwa walilazwa ni pamoja na pampasi na sabuni.

Naye Katibu wa Kituo cha Afya cha Halmashauri ya Chamwino na Kaimu Mganga Mfawidhi wa kituo hiko, John Daniel aliishukuru JKT kutokana na msaada walioutoa kwa wagonjwa pamoja na kufanya usafi wa mazingira akisema jambo hilo limeonyesha jamii kwamba JKT limekamilika kila idara.

Mbali na hilo alizitaka taasisi nyingine kuiga mfano wa jeshi hilo ambapo limetumia maadhimisho yao ya miaka 60 kufanya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kugawa zawadi kwa wagonjwa waliolazwa katika hospitali hiyo.

Akizungumzia kuhusu huduma wanazotoa katika hospitali hiyo alisema wanahudumia wagonjwa 320 kwa wiki, aliishukuru serikali kutokana na kuwekeza katika sekta ya afya.

# PPRA, TAKUKURU waingia makubaliano ya ushirikiano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wameingia makubaliano yanayolenga kupambana na vitendo vya rushwa kwenye eneo la ununuzi wa umma.

Akizungumza kwenye hafla hiyo jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakimu Maswi, alisema mwaka 2010 taasisi hizo kwa mara ya kwanza ziliingia makubaliano ya kitaasisi kushirikiana kwenye eneo hilo.

"Mahusiano haya yaliweka msingi wa kushirikiana ambao TAKUKURU iliwezeshwa na kufanya kazi taarifa zinazotolewa na PPRA zenye viashiria vya rushwa," alisema.

Maswi alisema ili kuongeza ufanisi wamepanua wigo wa ushirikiano ili kufanikisha vita ya rushwa kwenye ununuzi wa umma.

"Kwenye ununuzi wa umma ndiko kuliko na rushwa kubwa hivyo tunahitaji wenzetu wa TAKUKURU ambao wanautaalamu kuhusu rushwa watusaidie kwenye eneo hili," alisema.

Alisema PPRA ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa thamani ya fedha kwenye ununuzi wa umma na sheria inaitaka taasisi hiyo kuwapo na haki, ushindani na matumizi mazuri ya fedha za umma.

"Sheria inatutaka kuhakikisha kuna ufanisi wa ununuzi wa umma na kuweka viwango vya ununuzi wa umma ambavyo hivi karibuni tumeanza ujenzi wa mfumo mpya wa ununuzi unaoitwa NeST ambao kwa kiasi kikubwa tunategemea utatuwezesha kutekeleza jukumu la ununuzi kwa ufanisi mkubwa," alisema.

Alibainisha PPRA ina mamlaka ya kukagua mienendo ya taasisi kuhusu ununuzi ambazo kwa sasa zipo 864.

"Kufanya uchunguzi kwenye ununuzi wa umma na kuangalia kama kuna viashiria vya rushwa ni taaluma na kwa kuwa TAKUKURU wana uwezo wa kufanya uchunguzi, tukaingia nao makubaliano ili kufanya kazi hii muhimu," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni, alisema eneo la ununuzi wa umma limekuwa na tatizo la muda mrefu la rushwa.

"Eneo hili ukianzia Tume ya Jaji Warioba iliyofanya utafiti wa masuala ya rushwa ilionesha kwamba ununuzi wa umma una tatizo kubwa kwenye rushwa nadhani ilisababisha kuanzishwa kwa PPRA," alisema. Alisema wamekuwa na makubaliano ya muda mrefu na sasa wamepanua wigo wa kushughulika na rushwa.

"Rushwa kwenye ununuzi wa umma ni tishio kubwa katika taifa lolote na vitendo vya rushwa kwenye ununuzi wa umma vinafanyika katika maeneo mbalimbali kuanzia mchakato wa uandaaji vigezo vya zabuni hadi kufikia kumpata mzabuni," alisema.

Alieleza moja ya athari za rushwa kwenye zabuni ni kupunguza ufanisi na ubora wa miradi.

Alisema: "Rushwa inaleta pengo la usawa kwenye manunuzi, inaondoa imani ya wananchi kwa serikali iliyopo madarakani, inasababisha upandishwaji holela wa bei na kumwathiri mwananchi wa kawaida."



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akizindua Shule ya Msingi Bahi Mission baada ya kukamilika. Wilaya ya Bahi ilipokea kiasi cha Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya mbili zenye jumla ya vyumba 28, madarasa manne ya awali, majengo mawili ya utawala na vichomea taka. **PICHA: LULU MUSA**

# Serikali, sekta binafsi kukabiliana na maafa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI imeweka mikakati ya kuimarisha ushirikiano na sekta mbalimbali katika kukabiliana na maafa ili kuhakikisha wananchi wanaishi katika mazingira salama.

Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Meja Jenerali Charles Mbuge, aliyasema hayo juzi wakati akifungua kikao kazi cha wataalamu waliokutana kwa lengo la kuhuisha na kutafsiri mwongozo wa utekelezaji wa dhana ya afya moja.

Alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la mwingiliano wa binadamu, wanyama na mazingira ambao husababisha kutokea kwa magonjwa mbalimbali yanayotoka kwa wanyama na kwenda kwa binadamu, hivyo ipo haja ya kuwapo kwa ushirikiano wa sekta mbalimbali katika kujiandaa, kuzuia na kukabiliana na majanga hayo.

"Tunahuisha mwongozo huu kwa sababu ya mabadiliko ya sheria na kanuni za usimamizi wa maafa. Mwongozo huu ni muhimu katika kurahisisha ushirikiano wa kisekta ili kujenga na kuimarisha ustahimilivu wa jamii dhidi ya milipuko ya magonjwa na dharura zingine zenye madhara kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira," alisema.

Meja Jenerali Mbunge alisema kwa mujibu wa mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwamo ya Shirika la Chakula na (FAO), Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), Shirika la Afya ya Wanyama (WOAH) na Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP) kwa pamoja husisitiza ushirikiano wa sekta mbalimbali ili kuwa na mikakati na sera za pamoja katika kuimarisha afya ya binadamu, wanyama na mazingira.

Alisema ili kutekeleza dhana ya afya ni muhimu kuwa na miongozo mbalimbali ili kurahishisha uratibu na utendaji katika ngazi zote.

Aidha, alibainisha kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa ina wajibu wa kuratibu utekelezaji wa dhana ya afya moja kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya 2004, Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya Mwaka 2022 na kanuni zake za mwaka 2022 pamoja na Mkakati wa Afya Moja 2022-2027.



# Wakulima nafaka watakiwa kutumia teknolojia za kisasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa mazao ya nafaka mkoani Mbeya wametakiwa kutumia teknolojia za kisasa kwenye uzalishaji ili kuongeza ubora wa mazao hayo utakaokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje.

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda, alitoa ushauri huo juzi kwenye mkutano ulioandaliwa na Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC) Mkoa wa Mbeya.

Mkutano huo unaofanyika kwa siku tatu ukiwa na lengo la kuhamasisha wajasiriamali kuchangamkia fursa za soko la nafaka na mazao.

Mbali na wanawake hao wafanyabiashara, pia mkutano huo uliwashirikisha wadau mbalimbali wa biashara wakiwamo maofisa uvuvi, maofisa biashara wa halmashauri, maofisa kilimo, wakulima na wataalamu wa viuatilifu.

Mapunda alisema wakulima wanatakiwa kuhakikisha wanatunza kumbukumbu za mazao wanayozalisha ikiwa ni pamoja na aina ya mbolea na dawa wanazotumia kwenye mazao yao.

Alisema wanunuzi wa mazao huwa wanahitaji kujua baadhi ya taarifa muhimu zinazohusu mazao husika kulingana na mahitaji ya walaji wa mwisho na kwamba wakulima wengi hawana utaratibu wa kutunza kumbukumbu hizo.

"Mnunuzi wa soko la kimataifa anapokosa taarifa hizi muhimu huwa anaweza asinunuwe mazao ama anaweza akawa na mashaka na mazao yetu, kwa hiyo tunawafundisha wakulima wetu kutunza hizi kumbukumbu," alisema Mapunda.

Alisema wanapopata taarifa za mahitaji ya soko la mazao wanatumia taarifa hizo kuwajengea uwezo wakulima pamoja na maofisa ugani ili kuhakikisha taarifa hizo zinazingatiwa wakati wa uzalishaji.

Makamu Mwenyekiti wa TWCC Mkoa wa Mbeya, Rose Romanus, alisema chama hicho kinafanya kazi ya kuwaunganisha wanawake wajasiriamali na masoko ya kimataifa kwa ajili ya kuuza bidhaa mbalimbali yakiwamo mazao. Alisema wanashirikiana na Kampuni ya Tuzo ambayo inafanya biashara ya mazao mbalimbali kimataifa kwa lengo la kuwatafutia masoko wanachama wetu.

"Hii kampuni inanunua mazao ya kilimo, uvuvi, mafuta, mbegu na bidhaa zingine ambazo asilimia kubwa zinazalishwa na wanachama wetu, kwa hiyo tunawaunganisha na hii kampuni ili wachangamkie," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Tuzo Group, Dk. John Kashika, alisema kampuni hiyo ni muunganiko wa kampuni mbalimbali ambayo yanafanya biashara ya mazao kimataifa.

Alisema wananunua mazao ya wakulima kwa kuzingatia vigezo vya soko la kimataifa na hivyo akawataka wananchi kuzalisha mazao kwa kuzingatia vigezo hivyo vya soko la kimataifa.

"Tunachokifanya ni kuhakikisha tunawapatia elimu wakulima wetu, tunawasaidia kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao yao," alisema Kashika.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Adam Mhagama, aliwaasa wakulima na wajasiriamali kuhakikisha mafunzo yote wanayopata yanakuwa chanzo cha kubadilika kimaisha.

Alisema Mkoa wa Mbeya una fursa mbalimbali za kiuchumi ambazo wajasiriamali wakizichangamkia vizuri wanaweza kuinuka kiuchumi na wakawa moja ya makundi yenye uchumi mkubwa.




Ofisa Uvuvi wa Mkoa wa Mbeya, Adam Mhagama, akizungumza na washiriki wa Mkutano wa Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC) (hawapo pichani), uliofanyika juzi, kuwahamasisha wafanyabiashara wa mazao ya nafaka kuchangamkia fursa za masoko ya kimataifa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wakazi Mbarali waiomba NEC kuharakisha uchaguzi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BAADHI ya wananchi wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuharakisha mchakato wa uchaguzi mdogo kwa lengo la kuziba pengo lililoachwa na aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Francis Mtega baada ya kufariki.

Mtega alifariki mwishoni mwa wiki baada ya kugongwa na trekta ndogo wakati akiendesha pikipiki kuelekea shambani kwake katika eneo la Kibaoni Kata ya Ihahi wilayani humo.

Wakizungumza na Nipashe wakati wa kuaga mwili wa mbunge huyo juzi, wananchi hao walisema wanahitaji kupata mbunge mapema ili kuepuka kukosa mwakilishi wao bungeni kwa muda mrefu.

Mmoja wa wananchi hao, Feston Mnyalu alisema kutokana na katiba ya nchi ilivyo, muda uliobaki kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025 ni mkubwa, hivyo ni lazima uchaguzi mdogo ufanyike ili kupata mbunge mwingine.

Alisema mchakato huo ukifanyika mapema watapata mwakilishi mapema ambaye atakuwa anatekeleza yale yaliyotakiwa kutekelezwa na marehemu Mtega.

"Tulikuwa na mbunge ambaye alikuwa mpole na ambaye alikuwa anasikiliza matatizo yetu, sasa Mungu amemchukua kwa hiyo tunaiomba serikali ituharakishie mchakato wa kumpata mbadala wake," alisema Mnyalu.

Naye Judith Sanga alisema mbunge huyo alikuwa anawasaidia wananchi wake mambo mbalimbali ikiwemo kuwasaidia wakulima kuboresha mifereji ya umwagiliaji kwa kutumia fedha zake mwenyewe.

Alisema kifo chake kimekuwa ni pengo kwao na hivyo akaiomba serikali kuharakisha uchaguzi wa kumpata mbunge mwingine ambaye ataziba pengo hilo.

"Tunajua kwamba hatuwezi kupata mbunge ambaye atakuwa kama Mtega moja kwa moja lakini hata huyo atakayepatikana basi apatikane haraka," alisema Judhith.

Mwili wa Mtega uliagwa juzi wilayani Mbarali na kusafirishwa kwenda kuzikwa wilayani Ludewa katika Mkoa wa Njombe.

# RC ahimiza wananchi Mbeya kutembelea vivutio vya utalii

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo katika mkoa huo ili kujifunza na kuinua uchumi wao na wa taifa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa ushauri huo jana wakati akizungumza na wafanyakazi wa Shule za Feza za visiwani Zanzibar ambao wapo mkoani hapa kwa lengo la kutembelea baadhi ya vivutio.

Alisema vivutio vilivyopo mkoani Mbeya ni vizuri lakini vinatembelewa zaidi na watalii kutoka mataifa ya nje na watu kutoka mikoa mingine wakati wenyeji walitakiwa wawe mstari wa mbele kuvitembelea.

Alisema utalii ni moja kati ya sekta zinazoinua uchumi wa taifa kutokana na kuwa na fursa mbalimbali za kuingiza fedha ikiwa ni pamoja na viingilio pamoja na biashara ndogo zinazouzwa na wenyeji.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo pia kuzalisha bidhaa mbalimbali ambazo zitakuwa zinanunuliwa na watalii wanaotembelea vivutio vya utalii.

"Naushukuru sana uongozi wa shule hizi kwa kutambua vivutio vilivyopo katika mkoa wetu, tunawakaribisha sana Mbeya iko vizuri na tuna vivutio vizuri sana ndani ya mkoa huu," alisema Homera.

Vilevile aliwakaribisha watalii hao kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Wakulima (Nane nane) yanayotarajiwa kufanyika kwa mara ya kwanza jijini Mbeya kuanzia Julai 25 mwaka huu mpaka Agosti 8.

Kiongozi wa msafara wa watumishi hao, Rajab Juma Rajab alisema waliamua kutembelea vivutio hivyo vilivyopo katika Mkoa wa Mbeya kwa lengo la kuunga mkono filamu ya 'Royal Tour' iliyoandaliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya wanakusudia kutembelea vivutio vya utalii vitano ambavyo ni Ziwa Ngosi, Maporomoko ya Kaporogwe, Ziwa Kisiba na Fukwe za Ziwa Nyasa.

Alisema ziara za kitalii wataendelea kufanya katika mikoa mingine nchini kwa lengo la kuhamasisha Watanzania wengine kutembelea vivutio.

"Tunaamini kwamba ile filamu (Royal Tour) lengo lake ni kuhamasisha utalii ndani ya nchi yetu kwahiyo sisi pia tunaungana na Rais kuhamasisha shughuli hizo," alisema Mwalimu Rajab.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbeya Mjini, Clemence Mwandemba ambaye aliambatana na watalii hao alisema ziara hiyo itasaidia kuwahamasisha wananchi wa Mkoa wa Mbeya kupenda vitu vya nyumbani.

Alisema serikali imejitahidi kuweka mazingira rafiki kwa watalii wa ndani hasa kuweka viingilio vidogo kuliko vya wageni lakini bado Watanzania walio wengi hawahamasiki kutembelea.

Alisema utalii ni sehemu ya vyanzo vya uchumi na hivyo akawataka wananchi wa mkoa huo hasa wanaoishi jirani na vivutio hivyo kuwakarimu wageni ili wanufaike kiuchumi.

Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa yenye maeneo mbalimbali ya vivutio ikiwa ni pamoja na misitu ya asili na ya kupandwa, maporomoko na milima yenye mvuto.



## Dk. Mwinyi: Bima ya Takaful itaitangaza nchi kimataifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuanzishwa kwa bima ya takaful ni fursa kwa nchi kujitangaza kimataifa kama eneo bora kwa uwekezaji katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Amesema kwa muda mrefu bima hiyo imekuwa ikitumiwa katika nchi za Afrika, Ulaya, Asia ili kutoa fursa kwa biashara ambazo zinafuata misingi ya dini ya kiislamu kupata huduma za bima.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati wa hafla ya uzinduzi wa huduma ya bima inayofuata misingi ya kiislamu (takaful).

Alisema kupitia mfumo huu uwekezaji utakaofanywa kwa fedha zitokanazo na ada za bima, utafuata miongozo sahihi iliyowekwa ili kuhakikisha haziwekezwi katika mambo yanayokwenda kinyume na misingi ya kiislamu.

"Ni dhahiri kuwa uanzishwaji wa huduma hii mpya ni hatua nyingine muhimu katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi ili kuchochea maendeleo ya Shirika la Bima la Zanzibar," alisema.

Dk. Mwinyi alisema hiyo ni fursa nyingine kwa nchi kujitangaza kama eneo bora kwa uwekezaji katika mwambao wa Afrika Mashariki na kuweka misingi imara katika kuhakikisha wanatoa fursa kwa kampuni na watu binafsi kupata huduma hiyo mpya ya takaful.

Aidha, alisema wataalamu wa masuala ya bima wanaeleza kwamba takaful ni kiungo muhimu katika ukuaji wa huduma za fedha zinazofuata misingi ya kiislamu kwa sababu huduma hiyo hutoa fursa kwa benki ambazo tayari zinaendeshwa kwa misingi hiyo, kutoa huduma za bima jambo ambalo halikuwezekana kabla ya uanzishwaji wake.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Bima Zanzibar, Arafat Ally Haji, alisema kampuni ya ZIC Takaful inatoa huduma za bima kwa kufuata misingi ya dini.

Alisema kuwa uanzishwaji wa huduma hizo za takaful ni sehemu inayokwenda kukamilisha maeneo makuu matatu yanayohitajika katika kufuata misingi ya sheria katika uchumi wa nchi, kwamba huduma hizo zilianza nchini mwaka 2018.

Alisema kuwa lengo la kuanzisha huduma hiyo ni kuwapa fursa wananchi, wafanyabiashara na wawekezaji kuchagua huduma zinazokidhi mahitaji yao kwa ubora ule ule ambao bima imekuwa ikihudumia kwa zaidi ya miaka 50.

Alisema ni imani yake kwamba huduma hiyo itajenga taswira bora zaidi mbele ya wadau na kuimarisha uwezo wao katika miradi, biashara na mali za wawekezaji.

Kamishna kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware Abdalla, alipongeza Shirika la Bima Zanzibar kwa kuwa shirika la kwanza nchini la kutoa huduma ya takaful.

Alisema utaratibu huo utasaidia kuongeza wigo kwenye nchi na mfuko katika kukuza uchumi wa nchi.

Dk. Baghayo, alisema uchumi wa bima unakua hivyo ni vyema kwa wawekezaji kujitokeza katika eneo hilo kwani wapo wahitaji wengi na kuwahudumia wananchi kwa ufanisi mkubwa.

# Muswada Sheria ya Habari Zanzibar mbioni kukamilika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema kuwa inaendelea na mchakato wa kukamilisha Muswada wa Sheria ya Habari Zanzibar ambapo sheria hiyo itasaidia kulinda na kuheshimu uhuru wa habari.

Hayo yalisemwa jana na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, wakati akizungumza katika kongamano la wahariri wa vyombo vya habari kuhusu Siku ya Kiswahili Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka ifikapo Julai 7.

Alisema pia uwepo wa sheria hiyo utasaidia kuwapo kwa matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari.

"Mchakato wa kuupitia muswada huu unaendelea vizuri na matumaini yangu kuwa itapatikana sheria nzuri ambayo itawafanya waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao bila ya vikwazo," alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema muswada huo upo ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupitiwa kwa mara ya mwisho kabla ya kufikishwa katika Baraza la Wawakilishi.

"Muswada upo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unapitiwa ili unapoondoka huo usiwe na vifungu vinavyokinzana maana sheria hiyo ikishapita ndio imepita, hivyo ni vyema kama kuna kasoro kuziondoa mapema," alisema Waziri Tabia.

Waziri huyo alisema baada ya muswada huo kutoka kwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali utapelekwa katika Baraza la Mawaziri kabla ya kusomwa katika Baraza la Wawakilishi.

Aidha, alisema wanatarajia kuwa muswaada huo utasomwa katika kikao kijacho cha Baraza la Wawakilishi ili kujadiliwa.

Hivyo, aliwataka waandishi wa habari na wadau wa habari kuendelea kuwa na subira kuhusu mchakato huo na muda siyo mrefu sheria kamili itapatikana.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi (wa pili kulia), akiongoza hafla ya uzinduzi wa huduma ya bima inayofuata misingi ya dini ya Kiislamu (Takaful) inayotolewa na Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) kupitia kampuni yake tanzu ZIC Takaful jijini Zanzibar jana. Wengine ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Ali Suleiman Ameir (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZIC, Arafat Haji (kulia) na Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Tuwainue wajasiriamali, tuondoe ukosefu wa ajira'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema bado kuna umuhimu wa kutilia mkazo suala la kuwainua wajasiriamali ili kupunguza tatizo la ajira hasa kwa vijana.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya mashine za usarifu wa bidhaa za mazao ya mboga, matunda na viungo kati ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Wakala wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi Zaznzibar (ZEEA) na kukabidhi vyeti kwa wajasiriamali 40 waliopatiwa mafunzo na kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali Chuo cha Karume Mbweni.

Alisema safari ya kufikia ajira hizo inaanza kwao kupitia mafunzo waliyopatiwa ambayo ni chachu ya kuisaidia serikali katika kupunguza suala la ukosefu wa ajira na kupambana na umaskini.

"Mkiondoka hapa na ujuzi wenu na taaluma yenu mtakuwa mpo katika nafasi nzuri ya kufanya shughuli za uzalishaji," alisema.

Waziri Soraga alisema anafahamu matarajio ya wengi ni kuajiriwa katika sekta binafsi na serikali lakini ni ukweli usiopingika kuwa ajira nyingi zinapatikana kutokana na shughuli za uzalishaji.

Aidha alisema serikali ina mpango wa kujenga vituo vikubwa viwili ambavyo vitawahudumia wajasiriamali wengi zaidi kwa wakati mmoja Unguja na Pemba na dhamira yake ni kujenga vituo hivyo kwa kila wilaya.

Hivyo, aliwataka wajasiriamali kutumia fursa zinazotolewa na serikali katika kuwainua kiuchumi na kuomba wakala huo kuzitunza mashine hizo ili kudumu na kuwanufaisha vijana watakaokwenda katika chuo hicho.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZEEA, Juma Burhan Mohammed, alisema kituo hicho kimetekeleza miradi ya kuongeza thamani bidhaa za asali, viungo, matunda na mboga ambapo umewasaidia vijana 40 wakiwamo 27 wanawake na 13 wanaume.

Burhan alisema makabidhiano hayo ya mashine 18 yanatokana na juhudi za serikali katika kuwawezesha wananchi kupitia FAO na wizara ambazo zitasarifu matunda, mboga na viungo, kuchambua vitunguu saumu, kusanga mwani, karafuu na viungo vyote vikavu.

Hivyo, aliwataka vijana kujiajiri na kuwaajiri wengine ili kupunguza tatizo la ajira nchini na kuwa wajasiriamali wakubwa watakaofanya kazi katika viwanda vikubwa.

Mwakilishi kutoka FAO, Nyabenyi Tito, alisema shirika hilo litaendelea kushirikiana na serikali katika kuona vijana wa Zanzibar wanajiajiri na kujikwamua na umaskini.

Alisema kuwa lengo la kutoa mashine hizo zenye thamani zaidi ya Sh. milioni 89 anaamini zitasaidia kuwakwamua vijana katika kuzalisha bidhaa kupitia mazao na mboga yaliyokuwapo nchini ambazo zitawasaidia kupata soko la uhakika.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 66 OF 2023.**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FROWIN PAUL NYONI - DECEASES**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY JACQUELINE MOSES RUGALABAM**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN.369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20 Day of 7, 2023.
Dated at Dodoma this **4 day of 7, 2023.**

REGISTRY OFFICER

## KUPOTEA KWA VYETI



**AIKA FRANK NKYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0269/0002 kilichotolewa na Anwarite Girls Secondary School mwaka 2008. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0210/0502 kilichotolewa na Bigwa Sisters Seminary mwaka 2011. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**DAR/URA/RB/158330/2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 17 OF 2023**
**In the Matter of the Estate of the Late DANIEL YOHANA MNKANDE**
**And**
**In the Matter of Application for letters of administration by DOROTHEA DANIEL MNKANDE**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 24 day of July, 2023.
**Dated at Korogwe this 21 day of June, 2023.**

DISTRICT COURT TANZANIA KOROGWE
DISTRICT COURT
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KILOLO**
**Kituo cha MAZOMBE Mkoa IRINGA**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 04/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAMISI BAKARI LUKINDO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA LIGHTNES SIFAEL LEKEY**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 Mwezi 07 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 04 Mwezi wa 07 Mwaka 2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

FEDRICK ANDREA NYALUKE

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI NAMBA T249 AWW, CHESISI NAMBA ME06-5600439. YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA TUNAOMBA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAE JALADA NAMBA IRI/IRI/226871/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

MAKANZA COMPANY LIMITED anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili MC 142 DUT AINA YA KING. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Control number: 9910837581807.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No. 76 of 2023**
**In the matter of the Estate of the late DEUS KIJUU ALFRED**
**And**
**In the matter of an application for letters of administration by CHARLES NICHOLAUS MOLLEL of P O BOX 1249, DODOMA**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 65 of the probate Rules , G.N. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of AUGUST, 2023
**Dated at Dodoma this 5 day of 7 , 2023.**

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE I/C

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Dawa za kulevya zaingizwa Ikulu ya Marekani

**WASHINTON,** MAREKANI

UCHUNGUZI umebaini kuwa kitu cheupe kilichopatikana ndani ya Ikulu ya Marekani ya White House kuwa ni dawa za kulevya aina ya Cocaine.

Kulingana na viongozi wa huduma za siri za Marekani, walisema kitu hicho cheupe kilipatikana katika eneo la kazi wakati wa ukaguzi wa kawaida.

Wakati tukio hilo linatoke, Rais Joe Biden na familia yake walikuwa katika makazi mengine ya Camp David.

Ikulu ya White House ilifungwa kama tahadhari katika muda saa mbili na dakika 45 Jumapili baada ya maofisa wa huduma za ujasusi kupata unga mweupe ndani ya eneo la kazi la West Wing, msemaji wa Huduma za ujasusi Anthony Guglielmi aliambia BBC katika taarifa.

Guglielmi alisema idara ya zimamoto iliitwa haraka na kubaini kuwa mzigo huo sio hatari.

Alisema furushi hilo limetumwa kwa uchunguzi wa ziada na kwamba uchunguzi unaendelea, ikiwa ni pamoja na kubaini ni vipi mihadarati hiyo iliingia ndani ya Ikulu. **BBC**

# Dunia yakumbwa na hali ya joto zaidi

**NEWYORK,** MAREKANI

WASTANI wa hali ya joto duniani ilifikia kiwango cha juu zaidi Julai 3, mwaka huu na kufikia nyuzi joto 17 kwa mara ya kwanza.

Watafiti wa Marekani walisema rekodi hiyo mpya ilikuwa ya juu zaidi katika rekodi yoyote muhimu iliyowahi kurekodiwa kuanzia mwisho wa karne ya 19.

Wanasayansi wanaamini kuwa mchanganyiko wa tukio la hali ya hewa la asili linalojulikana kama El Niño na utoaji unaoendelea wa wanadamu wa hewa ya kaboni dioksidi ndio unaosababisha joto.

Mwezi uliopita pia umethibitishwa kuwa ndio mwezi Juni wenye joto zaidi duniani kuwahi kurekodiwa.

Wanasayansi katika Vituo vya Kitaifa vya Utabiri wa Mazingira wa Marekani walisema kuwa wastani wa joto duniani umefikia 17.01C tarehe 3 Julai, na kuvunja rekodi ya awali ya 16.92C ambayo ilikuwa katika kiwango hicho tangu Agosti 2016.

Tangu kuanza kwa mwaka huu, watafiti wamekuwa na wasiwasi juu ya kuongezeka kwa hali ya joto ardhini na baharini.

Rekodi ya joto la msimu wa vuli nchini Uhispania na nchi nyingi za Asia kuwa na mawimbi ya joto baharini katika sehemu ambazo kwa kawaida hayaonekani, kama vile Bahari ya Kaskazini.

Wiki hii China iliendelea kukumbwa na wimbi la joto la kudumu na hali joto katika baadhi ya maeneo ya juu ya 35C, wakati Amerika Kusini pia ikiripotiwa kuwa na hali mbaya ya joto.

Kiwango cha juu zaidi kilitokea Jumatatu ndicho cha joto zaidi tangu rekodi za ufuatiliaji wa satelaiti zilipoanza mwaka wa 1979. **BBC**

# Rais Kiir kujitosa uchaguzi wa kwanza Sudan Kusini

**JUBA, SUDAN** KUSINI

RAIS wa Sudan Kusini, Salva Kiir, ameahidi kuwania nafasi hiyo katika uchaguzi wa kwanza ambao umepangwa kufanyika mwaka ujao.

Kiongozi huyo ambaye ni kamanda mkuu wa wapiganaji wa msituni, amekuwa rais pekee wa taifa hilo tangu alipoliongoza kupata uhuru wake kutoka kwa Sudan mwaka 2011.

Kipindi cha mpito kilikusudiwa kuhitimishwa na uchaguzi mkuu mnamo Februari 2023, lakini hadi sasa serikali imeshindwa kufikia vifungu muhimu vya makubaliano, ikiwa ni pamoja na kuandaa katiba mpya.



"Ninakaribisha uidhinishaji wa kugombea urais mwaka 2024, tukio hilo litakuwa la kihistoria" Kiir aliwaambia wafuasi wa chama chake tawala cha Sudan People's Liberation Movement.

Kiongozi wa upinzani Kiir Riek Machar anatarajiwa kugombea urais katika uchaguzi ujao.

Hakuna mgombea mwingine ambaye ametangaza kugombea, lakini adui wa kihistoria Riek Machar anatarajiwa kugombea.

Mwezi Agosti, viongozi hao wawili waliongeza serikali yao ya mpito kwa miaka miwili zaidi ya muda uliokubaliwa, wakitaja haja ya kushughulikia changamoto zilizokwamisha utekelezaji wa makubaliano ya amani. **BBC**



Askari wa Israel akikagua gari katika kizuizi kilichowekwa ukingo wa Magharibi. **PICHA: DW**

# Jeshi la Israel laondoka Jenin

**JERUSALEM,** PALESTINA

WANAJESHI wa Israel wameondoka kwenye ngome ya wanamgambo Wakipalestina iliyoko Ukingo wa Magharibi, lakini wameonya operesheni yao dhidi ya wanamgambo haijamalizika.

Katika operesheni hiyo kubwa ya kijeshi, watu wanane wajeruhiwa katika shambulio la gari katika mji watelaviv apalestina 12 na mwanajeshi mmoja wa Israel wameuawa katika mji wa Jenin.

Wakazi wa kambi ya wakimbizi ya Jenin jana wametoka majumbani mwao kushuhudia uharibifu uliofanywa na jeshi la Israel, ikiwamo mrundikano wa vifusi na magari yakiwa yametiwa moto.

Wenye maduka wameanza kusafisha uharibifu huku matingatinga nayo yakiingia kazini kuondoa vifusi.

Maelfu waliokuwa wamekimbia vita wameanza kurejea, baadhi walikuwa wakijiandaa kufanya maziko ya kishujaa ya waliouawa huku wengine wakijaribu kufanya ukarabati wa kambi ya wakimbizi ya Jenin ambayo ndiyo kambi kongwe kabisa ikiwa na miaka 75.

Jeshi la Israel lilisema limewalenga wanamgambo pekee kwenye operesheni yake hiyo ya saa 48 iliyokuwa na lengo la kuiharibu kabisa miundo mbinu ya wanamgambo Wakipalestina.

Aidha, Jeshi hilo limedai kuyasambaratisha kwa kiasi kikubwa makundi ya wanamgambo kwenye operesheni hiyo iliyohusisha msururu wa mashambulio ya anga.

Hata hivyo bado haijulikani ikiwa kutakuwa na athari zozote za muda mrefu na hasa baada ya mwaka mmoja na nusu tangu kutokea vita vikubwa katika eneo hilo la Ukingo wa Magharibi.

Kabla ya jeshi hilo la Israel kuondoka jana, waziri mkuu Benjamin Netanyahu aliapa kuwa yupo tayari kuamrisha operesheni nyingine kubwa kama hiyo ikilazimika.

"Yeyote anayefikiria kwamba shambulio kama hili litatuzuia kuendelea na mapambano yetu dhidi ya ugaidi anakosea, watakuwa hawajui mwamko wa dola la Israel, hawajui serikali yetu, raia wetu au wapiganaji wetu. Nawapongeza wapiganaji wetu shupavu walioharibu miundombinu mingi ya magaidi katika mji wa Jenin na kwa hivyo kuzuia mashambulizi mengi," alisema. **DW**

# BARRICK NORTH MARA RUNNERS KUSHIRIKI CAPETOWN MARATHON

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashindano ya riadha yanazidi kuwa na mwamko mkubwa nchini, yakijumuisha watu wenye umri wa rika mbalimbali, klabu mbalimbali za marathon zimezidi kuanzishwa na baadhi yake zinazidi kuwa tishio kutokana na kuwa na wachezaji wenye vipaji vikubwa.

Barrick North Mara Runners Club, inayoundwa na wafanyakazi wa mgodi wa Barrick wa North Mara, ni moja ya timu ambayo inazidi kuja juu kwa kasi ambapo kwa sasa ipo kwenye maandalizi ya kwenda kushiriki, Capetown Marathon 2023 kwenye mbio za kilometa 42.

Mbio hizo zinatarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu nchini Afrika Kusini, ambapo nahodha wa timu hiyo, Sarah Cyprian, hivi karibuni, alisema klabu hiyo iliyoanzishwa mwaka 2016 inajumuisha wakimbiaji 66, miongoni mwao wanaume ni 53 na wanawake 13, ipo tayari kwenda kushiriki mbio hizo Afrika Kusini.

Alisema baadhi ya mashindano ambayo klabu hiyo imeshiriki ni Kilimanjaro International Marathon - mjini Moshi, Capital City Marathon - jijini Dodoma ambapo ilitoa mshindi wa tisa wa umbali wa kilometa 21, Serengeti Migration Marathon kilometa 21, Serengeti Safari Marathon km. 21-Lamadi na Lake Victoria Marathon -jijini Mwanza huku nako ikitoa mshindi wa nne kwa wanawake umbali wa kilometa 21.

Mashindano makubwa ambayo timu hiyo imeshiriki na kung'ara ameyataja kuwa ni Kilimanjaro International Marathon ambapo ilishiriki mbio za kilometa 21 na kilometa 42. Kwa mbio hizo za masafa marefu ya kilometa 42 klabu iliwakilishwa na nahodha huyo mwenyewe.

Akielezea siri ya mafanikio ya klabu hiyo, Sarah alisema:"Kampuni ya Barrick inayo sera madhubuti katika kusaidia wafanyakazi kwenye upande wa michezo. Kwanza kwa kuwa na miundombinu ya mazoezi kama gym, swimming pool, uwanja wa mpira wa miguu, uwanja wa mpira wa kikapu pamoja na uwanja wa mpira wa pete.

"Pia inatoa vifaa na nyenzo mbalimbali za kufanyia mazoezi, vilevile kugharamia huduma zote tunapoenda kwenye mashindano nje".

Aliongeza kusema kuwa kampuni pia kupitia Kitengo cha Afya na Usalama huwa inaandaa mashindano ya ndani kwa kushindanisha idara mbalimbali hiyo ikiwa kama njia mojawapo kuweka vizuri afya za mwili na akili za wafanyakazi wawapo kazini.

Kuhusu namna wanavyoweza kutenga muda wa kazi na wa kufanya mazoezi, Sarah alisema: "Kila mtu ana saa 24 katika siku. Klabu ya North Mara Runners huwa tunatenga muda wa saa moja kwa siku kufanya mazoezi. Mazoezi hayo huwa tunafanya jioni baada ya kutoka kazini, na mara chache ratiba zinapokuwa zinabana jioni huwa tunafanya mazoezi saa kumi alfajiri kabla ya kwenda kazini".




Baadhi ya wanariadha wa Barrick North Mara Runners Club wakifurahi baada ya kumaliza kushiriki kukimbia mbio za Lake Victoria Marathon zilizofanyika jijini Mwanza hivi karibuni. **MPIGAPICHA WETU**

## ZFF yavunja kambi Wanawake U-18

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), limevunja kambi ya Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya umri wa miaka 18 (U-18), iliyotarajiwa kushiriki michuano ya CECAFA chini ya umri huo nchini Kenya, imeelezwa.

ZFF imefikia uamuzi huo baada ya michuano hiyo kuendelea kupigwa kalenda ambapo hadi sasa bado haijatangazwa tarehe nyingine ya michuano hiyo baada ya kusogezwa mbele mara mbili.

Akizungumza na gazeti hili jana visiwani hapa, Katibu wa Kamati ya Maendeleo ya Soka la Wanawake Zanzibar, Khatma Mwalim, alisema kutokana na kuahirishwa kwa michuano hiyo mara mbili kwa tarehe zilizotolewa hapo awali, wameona ni bora kuwarejesha wachezaji hao majumbani mwao.

Alisema wachezaji ni wadogo kulingana na umri walionao, huku baadhi wakiwa bado wanaendelea na masomo, hivyo wameona bora kuvunja kambi ili kutoa fursa kwa wanaosoma kwenda kuendelea na masomo yao na wachezaji wengine kurudi katika timu zao ili kujiandaa na msimu mpya wa ligi.

Alisema mbali na kuongezeka kwa gharama za kambi, lakini kwa tamaduni si busara kuendelea kukaa kwa muda mrefu hasa ikizingatiwa wale ni watoto wa kike.

"Tumeamua bora kuvunja kambi ambayo tumekaa kwa takriban mwezi mmoja na nusu, mbali na kuongezeka kwa gharama za kambi, lakini pia kukaa muda mrefu na watoto wakike si busara. Mbali na mpira, lakini watoto wa kike bado wanahitajika nyumbani kufanya shughuli za kuwasaidia wazazi,"alisema.

Alisema iwapo itatolewa tarehe nyingine ya kuchezwa mashindano hayo, wataweka kambi ya muda mfupi ya kujiandaa na safari.

# Mwakinyo kuwania Mkanda wa WBO

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, anatarajia kupanda ulingoni kuwania mkanda wa Dunia wa WBO chini ya Kampuni ya Promosheni ya Ngumi za Kulipwa nchini, PAF Promotion Entertainment Company LTD, katika pambano litakalopigwa Agosti mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Hassan Mwakinyo alisema kwa sasa amejipanga kuhakikisha anakata kiu ya Watanzania katika mchezo wa ngumi za kulipwa kwa kucheza pambano la mkanda ambao hajawahi kuuwania akicheza nchini.

Alisema baada ya kukosekana ulingoni kwenye ngumi za ushindani, sasa anarudi upya kwa kupanda ulingoni katika pambano hilo la kuwania mkanda wa Ubingwa wa Dunia wa WBO.

"Muda mrefu nilikuwa natamani nipate pambano kama hili, lakini nilikuwa bado sina vigezo, sasa nashukuru nimevipata na utakuwa wakati mzuri sana kwangu kupata pambano hili. Ningefurahi pia kwa mabondia wa Tanzania na wao wangepata nafasi kama hii tena wakipigana hapa hapa nchini, lakini bado vigezo hawana," alisema na kuongeza:

"Ukimya wangu haukuwa wa bure, nitakidhi kiu ya mashabiki wangu ambao hawajaniona muda mrefu ulingoni. Nitawapa furaha mashabiki wangu. Nimejiandaa na bado najiandaa vema mpaka sasa kwa pambano hilo.

"Kwa Tanzania bondia yeyote anayetaka kupigana na mimi kwanza agombee mkanda huu ninaokwenda kuupigania. Lakini kama kuna bondia anataka hivyo aje Masaki tupigane," alisema Mwakinyo.

Naye Promota wa pambana hilo, Fadhili Maogola, alisema wakati Mwakinyo akifanya mazoezi kujiandaa na pambano hilo, wao wako katika mchakato wa kumtafutia mpinzani mzuri ambaye atampa ushindani.

"Kwa sasa ni mapema kumweka wazi mpinzani wake kwa sababu tuko kwenye mazungumzo na kuangalia bondia gani ambaye anaweza kumpa ushindani mkubwa Mwakinyo ambaye amekuwa na rekodi nzuri katika ngumi," alisema Maogola.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SILVA KUPELEKWA SOKONI
KLABU ya Manchester City iko tayari kukubali dau la kati ya pauni milioni 45 na milioni 50 msimu huu wa majira ya joto kwa ajili ya winga wa Ureno, Bernardo Silva, 28. **(Football Insider)**

### GUEHI AWANIWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United ina nia ya kutaka kumnunua beki wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 22, ingawa Crystal Palace inataka ada ya takriban pauni milioni 60. **(Football Insider)**

### ALCANTARA AVUTIA SAUDIA
THIAGO Alcantara anazivutia Klabu za Saudi Arabia, ingawa Liverpool bado haijapokea ofa rasmi ya kumnunua kiungo huyo wa kati wa Hispania mwenye umri wa miaka 32. **(Times)**

### ROQUE AKUBALIWA BARCA
BARCELONA imekubali dili la kumsajili, Vitor Roque kutoka Athletico Paranaense, lakini lazima ione kama inaweza kupunguza bili yao ya mshahara kabla ya kujua kama mshambuliaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 18, anaweza kujiunga na msimu huu wa majira ya joto, Januari au msimu ujao. **(Sport)**

### GLOUKH KWA CITY, ARSENAL
ARSENAL, Manchester City, Manchester United na Tottenham Hotspur, ni miongoni mwa klabu kubwa ambazo zimeonesha nia ya kumnunua kiungo wa Red Bull Salzburg, Israel Oscar Gloukh,19. **(Guardian)**

### SANCHEZ ALENGWA UNITED
GOLIKIPA wa Brighton raia wa Hispania, Robert Sanchez mwenye umri wa miaka 25, ameibuka kama shabaha inayolengwa na Manchester United**. (Mail)**

### RICE SAFI ARSENAL
MPANGO wa Arsenal wa kumsajili kiungo wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24, kwa ada ya pauni milioni 105, unakaribia kukamilika, huku sehemu ya ada hiyo ikitarajiwa kulipwa kwa awamu tatu. **(Guardian)**

### BARCA KUIPIKU MADRID
BARCELONA imeitangulia Real Madrid katika kinyang'anyiro cha kumnunua Arda Guler wa Uturuki kutoka Fenerbahce, huku AC Milan na Borussia Dortmund zikiachana na harakati zao za kumnasa kiungo huyo mshambuliaji mwenye umri wa miaka 18. **(Sport)**

### BEI YA MARTINEZ YATAKIWA
REAL Madrid imeitaka Inter Milan kutaja bei ya kumnunua mshambuliaji wa Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 25. **(Sport)**

### BASSEY ATAKIWA BRIGHTON
KLABU ya Brighton imeongeza juhudi yao ya kumnunua beki wa Ajax na Nigeria, Calvin Bassey mwenye umri wa miaka 23, kama mbadala wa mlinzi wa Chelsea, Levi Colwill, 20. **(The Athletic)**

### TOURE ATAJWA ALMERIA
KLABU ya Almeria imesema Everton na klabu mbili za Italia zimewasilisha ofa ya kumnunua mshambuliaji wa Mali, El Bilal Toure, 21. **(Diario de Almeria)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# FIRMINO NAYE ASAJILIWA RASMI AL AHLI YA SAUDIA

●●●Ni baada ya kumaliza mkataba Livepool, sasa kukipiga na Edouard Mendy...

**JEDDAH, Saudi Arabia**

ROBERTO Firmino amejiunga na Klabu ya Al Ahli ya Saudi Arabia kama mchezaji huru baada ya mkataba wake na Liverpool kumalizika mwishoni mwa msimu uliopita, ilitangazwa jana.

Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 31, amekubali kusaini mkataba wa miaka mitatu na timu ya Saudia na anajiunga na kipa wa zamani wa Chelsea, Edouard Mendy katika klabu hiyo yenye maskani yake Jeddah.

Fowadi huyo wa Brazil alikaa Anfield kwa miaka nane, akifunga mabao 110 katika michezo 361.

Firmino alishinda mataji saba akiwa na Liverpool ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019 na taji la kwanza kabisa la Ligi Kuu ya England kwa kipindi cha miaka 30, mwaka 2020.

Klabu za Saudi Arabia zimefuata mkakati mkali wa kusajili wachezaji kutoka Ulaya katika miezi ya hivi karibuni.

Wamekuwa wakiwashawishi baadhi ya wachezaji wenye majina makubwa kusaini mikataba yenye faida na timu za nchi hiyo - Cristiano Ronaldo alijiunga na Al Nassr Januari na Karim Benzema aliondoka Real Madrid na kujiunga na Al Ittihad mapema mwezi huu.

Al Ahli ilishinda taji la Ligi ya Daraja la Kwanza la Saudi Arabia msimu uliopita na kufanikiwa kupanda tena kwenye Ligi Kuu ya Saudi Pro kwa ajili ya msimu wa 2023-24.

# BRAZIL YAMTANGAZA KOCHA WA MUDA WAKIMSUBIRI ANCELOTTI



**RIDO DE JANEIRO, Brazil**

KOCHA wa Klabu ya Fluminense, Fernando Diniz, ameteuliwa kuwa kocha mkuu wa muda wa Timu ya Taifa ya Brazil huku wakimsubiri Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti.

Diniz mwenye umri wa miaka 49, alifikia makubaliano hayo juzi na Shirikisho la Soka la Brazil (CBF), kuiongoza timu ya taifa kwa mwaka mmoja, wakati huo huo akiendelea na majukumu yake katika Klabu ya Fluminense.

"Ni ndoto kwa mtu yeyote, heshima na fahari kubwa kuweza kuitumikia timu ya taifa," alisema Diniz baada ya kutangazwa rasmi.

"Kwa kweli ni wito, kazi ya pamoja ya CBF na Fluminense. Nina imani kubwa kwamba tunaweza kulipeleka mbele jambo hili na kulifanyia kazi."

Rais wa CBF, Ednaldo Rodrigues, hivi karibuni alisema Ancelotti, ambaye yuko chini ya mkataba na Real Madrid hadi Juni 2024, anabaki kuwa chaguo lao la kwanza kuiongoza timu ya taifa kwenye Kombe la Dunia la 2026.

Licha ya kutakiwa na Brazil katika miezi ya hivi karibuni, Ancelotti alisisitiza nia yake ya kuendelea kuwa kocha wa Real Madrid hadi mkataba wake utakapomalizika.

Brazil ambao ni mabingwa mara tano wa Kombe la Dunia, wamekuwa bila kocha kwa muda tangu Tite ajiuzulu baada ya kutolewa kwao robo fainali kwenye Kombe la Dunia la 2022 Desemba. Kocha wa Brazil chini ya umri wa miaka 20, Ramon Menezes, aliiongoza timu ya taifa tangu wakati huo.

Diniz amekuwa Fluminense tangu Aprili 2022 na yuko chini ya mkataba na klabu hiyo hadi Desemba 2024.

Ataanza kuifundisha rasmi Brazil kwenye mchezo wake wa kwanza wa kufuzu Kombe la Dunia nyumbani dhidi ya Bolivia Septemba 4, mwaka huu.

Brazil itacheza mechi nyingine tano za kufuzu Kombe la Dunia kati ya Septemba na Novemba 2023, ikifuatiwa na mapumziko hadi Septemba 2024. Mipango pia imetangazwa kwa mechi ya kirafiki na Hispania, Machi 2024.

Mashindano ya Copa America yanatarajiwa kufanyika kati ya Juni na Julai 2024, nchini Marekani na CBF wanatarajia kuwa na Ancelotti kufikia wakati huo.

Kocha huyo wa Italia, ameziongoza kwa nyakati tofauti Juventus, AC Milan, Chelsea, Paris Saint-Germain na Real Madrid katika maisha yake ya ukocha kwa miaka 28 na kuwa kocha pekee kushinda Ligi ya Mabingwa mara nne - lakini hajawahi kuinoa timu yoyote ya taifa.

# Neymar apigwa faini dola milioni 3 kuharibu mazingira

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Neymar, ametozwa faini ya dola milioni 3.33 na mamlaka ya nchini Brazil kwa kukiuka kanuni za mazingira za eneo la Pwani ambapo amejenga jumba lake la kifahari katika Jiji la Mangaratiba nje ya Rio de Janeiro.

Mamlaka ya Jiji la Mangaratiba ilisema katika taarifa yake kuwa imetoa faini nne baada ya Neymar kushtakiwa kwa kujenga ziwa bandia katika jumba lake la kifahari kinyume cha sheria.

Hata hivyo, wasemaji wa Neymar mwenye umri wa miaka 31, walikataa kutoa maoni yoyote kwa vyombo vya habari.

Neymar anaweza kukata rufani dhidi ya uamuzi huo, ambao utakabidhiwa kwa polisi kwa uwezekano wa kufunguliwa mashtaka.

Juni 22, maofisa wa mazingira walikagua nyumba ya Neymar baada ya malalamiko yaliyotolewa, ambayo yalionesha kazi kubwa ya ujenzi iliyofanywa bila idhini ya mazingira.

Mamlaka ya Jiji la Mangaratiba ilisema katika taarifa yake kwamba makosa kadhaa ya mazingira yalifanywa "katika ujenzi wa ziwa bandia kwenye jumba hilo."

Miongoni mwa ukiukwaji huo ni pamoja na kuzuia na kuchepusha maji ya mto bila kibali, kusogezwa kwa ardhi na kukandamiza mimea bila idhini.

"Idara ya Mazingira, pamoja na kutumia faini hizo kwa kuzingatia uharibifu wa mazingira uliotokea, imetoa taarifa kwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Polisi, Polisi wa Ulinzi wa Mazingira na Vituo vingine vya udhibiti wa mazingira," ilisema taarifa hiyo.

Kampuni iliyojenga ziwa hilo la bandia, Genesis Ecossistemas, ilisherehekea kazi hiyo kwenye chaneli zake za mitandao ya kijamii. Ilisema ziwa hilo lina ukubwa wa mita za mraba 1,000.

Kampuni hiyo ilitoa taarifa kwenye Instagram ikisema kwamba itatafuta kibali kinachohitajika na kufanya kazi na serikali kutii kanuni hizo.

# Mount athibitisha kuondoka Chelsea

**LONDON, England**

MASON Mount amethibitisha kuwa ataondoka Chelsea baada ya miaka 18 katika klabu hiyo.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24, alijiunga na timu hiyo pale kwenye dimba la Stamford Bridge baada ya kuhitimu kutoka akademi ya klabu hiyo.

Tangu aanze kucheza mechi yake ya kwanza mwaka 2019, amefunga mabao 27 na kutoa pasi za mabao 22 katika mechi 129 za Ligi Kuu.

Na huku Manchester United ikikaribia kukamilisha usajili wake, Mount aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram jioni kuwaaga 'The Blues' hao.

Alisema: "Habari mashabiki wa Chelsea, kutokana na uvumi uliokuwapo katika kipindi cha miezi sita iliyopita huenda jambo hili lisiwashangaze.

"Lakini haifanyi iwe rahisi kuwaambia kuwa nimefanya uamuzi wa kuondoka Chelsea.

"Ninahisi mnastahili zaidi ya taarifa iliyoandikwa, kwa hivyo nilitaka kuwaambia moja kwa moja shukrani zangu kwenu kwa msaada wenu wote kwa miaka 18 iliyopita.

"Najua baadhi yenu hamtafurahishwa na uamuzi wangu, lakini ndio sahihi kwangu wakati huu katika kazi yangu.

"Nilijiunga na Chelsea nikiwa na umri wa miaka sita na tumepitia mengi pamoja.

"Kushinda Kombe la Vijana, Tuzo za Mchezaji Bora wa Mwaka, Kombe la Super Cup, Kombe la Klabu Bingwa Dunia na bila shaka usiku usiosahaulika tuliposhinda Ligi ya Mabingwa Ulaya."



HABARI MICHEZO

# BODI YA LIGI YAKOMALIA WACHEZAJI KUPIMWA AFYA

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), imezitaka klabu zote za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship na Daraja la Pili 'First League' kuwafanyia vipimo vya afya wachezaji wote watakaowatumia kwa msimu wa mashindano wa 2023/24 ili kutelekeza matakwa ya kikanuni na masharti ya leseni za klabu.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi hiyo, imesisitiza kuwa wachezaji wote watakaotumika kwa michezo ya ligi msimu ujao wanapaswa kuwa wamepimwa na kuthibitishwa na daktari kuwa hawana matatizo yoyote yanayoweza kuhatarisha usalama wao na wachezaji wengine.

"Wachezaji ambao hawatofanyiwa vipimo vya afya na kupata cheti cha utimamu wa afya, watakosa sifa za kusajiliwa na kupatiwa leseni maalum za usajili wa wachezaji zinazotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), hivyo hawatoruhusiwa kucheza mashindano yoyote yaliyo chini ya shirikisho hilo," ilisema taarifa hiyo.

Ilisema zoezi hilo ni muhimu na la lazima kwa mujibu wa Kanuni ya 69:2 (2.4) ya Ligi Kuu, na ya 70:2.(2.4) kwa Kanuni ya Ligi ya Championship na First League kuhusu maombi ya usajili, hivyo klabu zote zinapaswa kuhakikisha zoezi hilo linafanyika kikamilifu chini ya daktari mwenye sifa na vigezo vinavyohitajika, huku ikizitakia klabu zote maandalizi mema ya msimu wa 2023/24.

Tayari Klabu ya Simba ilianza kuwapima wachezaji wake tangu Jumatatu iliyopita kwenye Hospitali ya Rufaa Muhimbili, huku Azam FC yenyewe ikianza zoezi hilo kwenye Hospitali ya Aga Khan, zote za jijini Dar es Salaam.



Wachezaji wa Yanga wakielekea Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam jana tayari kwa safari ya Malawi kwenye maadhimisho ya sherehe za uhuru wa nchi hiyo. Leo watacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Nyasa Big Bullets ya nchini humo. **MPIGAPICHA WETU**

# CAF sababu JKU kumtema kocha wao wa mafanikio

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya JKU imemtambulisha Kocha Salum Ali Haji kuwa kocha wake mkuu atakayeinoa kuelekea msimu mpya wa Ligi wa 2023/2024 baada ya kuachana na Sheha Khamis.

JKU ni wawakilishi wa Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kwa msimu ujao baada ya kuibuka bingwa wa michuano ya Kombe la ZFF (FA Cup) kwa msimu wa 2022/2023.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Shazil Khatib, alisema wamefanya mabadiliko hayo ya kocha mkuu ili kulingana na vigezo vya CAF katika ushiriki wao wa michuano ya kimataifa.

Alisema kocha huyo mpya ambaye ataenda kukinoa kikosi hicho, amekidhi vigezo vya CAF kwa kuwa na Leseni A inayotambulika na shirikisho hilo.

Alisema anatumia mabadiliko hayo madogo ya benchi la ufundi yaliyofanywa na uongozi wa timu hiyo, yamelenga kuhakikisha wanafanya vizuri katika michuano hiyo ya kimataifa pamoja na Ligi Kuu Zanzibar katika msimu mpya.

Aidha, alisema wataendelea kukumbuka mchango wa kocha wao wa zamani kwa kuifundisha timu hiyo kwa mafanikio makubwa hadi kutwaa Kombe la FA.

"Timu ya JKU itaendelea kuthamini mchango mkubwa wa kocha wetu ambaye tumeachana naye, yeye ndio chachu ya mafanikio yetu mpaka kufikia hapa tulipo, hivyo tunamtakia mafanikio katika timu yoyote aendayo na tutashirikiana naye," alisema.

Hata hivyo, alisema timu hiyo ipo mbioni kumtambulisha ofisa habari wake pamoja timu yake nzima ya kitengo cha habari ili kuendana na sheria ya leseni za klabu.

## Yanga yataja masharti 3

INATOKA UK. 24

Kigamboni.

Hata hivyo, akizungumzia kuondoka kwa Mayele, rais wa Yanga, Hersi Said, alisema ni mchezaji bora na wanayofuraha kuona anahusishwa na timu nyingine, jambo ambalo linaonesha kuwa Yanga ni timu kubwa na ina wachezaji wakubwa huku akitaja mambo matatu yatakayofanya kumruhusu kuondoka.

"Kama atakuwa anataka kuondoka, tutaangalia vitu vitatu, moja tutataka kumbakiza, mbili tutaangalia bei nzuri, tatu ni nani atachukua nafasi yake," alisema Hersi.

Aliongeza kuwa wako makini kuhusu wachezaji wao na wanaendela kufanya usajili mzuri baada ya kufanikiwa kumsainisha mkataba wa miaka miwili, beki kutoka Singida Fountain Gate FC, Nickson Kibabage.

Hersi alisema usajili wa nyota huyo ni mwanzo na kuahidi makubwa yanakuja baada ya kufanya usajili mzuri wa kimataifa.

Alisema Kibabage ni sehemu ya usajili wao uliopendekezwa na benchi lao la ufundi na kuamini atakuja kuwasaidia na kupata uzoefu mkubwa katika maisha yake mapya ndani ya Yanga.

"Kibabage ni miongini mwa usajili wetu bora wa wachezaji wazawa kwa sababu amepita katika ngazi zote za mchezaji anapoanzia, tumefanya usajili mzuri na tumeanza na huyo, wengine wanakuja," alisema Hersi.

Kuhusu safari yao kuelekea Malawi ambapo kikosi kiliondoka jana, baada ya kupata mwaliko kutoka serikali ya nchi hiyo, Hersi alisema ni heshimu kubwa kwa klabu hiyo, na kwamba leo watashuka dimbani dhidi ya Nyasa Big Bullets kucheza mechi ya kirafiki.

## Simba yatangaza kiraka Mcameroon

INATOKA UK. 24

Ahmed Ally, alisema hiyo ni dibaji tu kwani wataendelea kushusha vyuma vingine kwa kuwa tayari wana orodha mkononi.

"Hiyo naweza kusema ni dibaji, au mvua ya rasharasha, tutaendelea kushusha vyuma, kutambulisha wachezaji na si wachezaji tu, bali bora watakaokuja kuisaidia na kuibeba timu kwenye mashindano yote ambayo klabu hii itacheza msimu huu, ikiwamo Super League, ukicheza michuano mikubwa kama hii, ni lazima pia uwe na wachezaji wa aina hiyo na si wa kuokoteza," alisema Ahmed.

Mchezaji huyo ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili, msimu uliopita aliibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu Rwanda akiwa na magoli 16 na asisti 5, lakini ni Mshindi wa Tuzo ya Mchezaji Bora wa Msimu nchini Rwanda, MVP.

Mbali na mchezaji huyo, klabu hiyo inadaiwa tayari imeshamalizana na baadhi ya wachezaji ambao inatarajia kuwatangaza wakati wote, nao ni beki wa kati, Che Fondoh Malone kutoka Cotonsport ya Cameroon, kipa Mbrazil, Caique Luiz Santos alikuwa akikipiga Ypiranga ya kwao Brazil na Fabrice Ngoma kutoka Al Hilal ya Sudan.

Pia ilikuwa na mazungumzo na wachezaji watatu viungo wakabaji, lengo likiwa ni kumpata mmoja, nao ni Efoe Novon kutoka ASKO Cara ya Togo, Harvy Ossete raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo anayeichezea FC Saint Eloi Lupopo, na Banfa Sylla wa MAS Fes ya Morocco.

Michezo

Alhamisi Julai 6, 2023
Nipashe



Firmino asajiliwa Al Ahli ya Saudia UKURASA 21

# YANGA YATAJA MASHARTI MATATU MAYELE KUONDOKA

●●●Ni baada ya kukataa milioni 408, Waarabu wamvuruga kichwa, timu kushuka dimbani leo...

**Na Saada Akida**

HUKU juhudi za Yanga kumshawishi mshambuliaji wao hatari, Fiston Mayele, kusaini mkataba mpya, zikigonga tena mwamba, klabu hiyo imetaja mambo matatu yanayoweza kuifanya sasa kumruhusu kuondoka.

Mayele ambaye bado ana mkataba wa mwaka mmoja na Yanga, anataka kuruhusiwa kuondoka kutokana na ofa nono alizowekewa mezani na klabu zaidi ya tatu za Uarabuni.

Tayari Yanga imeelezwa pamoja na kumshawishi Mayele kuwa ipo tayari kumwongezea mshahara kutoka Sh. milioni 23 walizokuwa wakimlipa mpaka milioni 34 kwa mwezi ili kumbakisha ambazo zingemfanya ndani ya mwaka mmoja kuvuna jumla ya Sh. milioni 408, lakini mshambuliaji huyo raia wa DR Congo ameweka ngumu na anachotaka kwa sasa ni kuruhusiwa tu kuondoka.

Kwa mujibu wa taarifa zilizolifikia Nipashe jana, Mayele ambaye alijiunga na Yanga mwaka juzi kwa mkataba wa miaka mitatu, amepata ofa nzuri kutoka Klabu ya Esperance ya Tunisia, Zamalek na Pyramids zote za Misri.

Chanzo chetu makini ndani ya Yanga kimeeleza kuwa Mayele na uongozi wa Yanga wamekaa vikao visivyopungua vitatu kutaka kumshawishi nyota huyo kusalia ndani ya timu hiyo, lakini mambo yamegonga mwamba.

"Mayele amewakomalia viongozi akitaka aruhusiwe kuondoka licha ya kupewa ofa ya kuongezewa mshahara kutoka milioni 24 hadi 34, lakini ameonesha msimamo wake wa kutaka kuruhusiwa kwenda moja ya timu walizompa ofa kubwa," kilieleza chanzo chetu.

Kiliongeza kuwa bado mazungumzo yanaendelea baina ya mchezaji huyo na viongozi, lakini mshambuliaji huyo amebeba vitu vyake vyote kutoka katika kambi ya timu hiyo, Avic Town,

UKURASA. 23



## Simba yatangaza kiraka Mcameroon

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imemtambulisha mchezaji wake wa kwanza mpya, 'kiraka' Mcameroon Willy Essomba Onana, aliyesajiliwa akitokea Klabu ya Rayon Sport ya Rwanda.

Mchezaji huyo mwenye sifa ya kucheza nafasi zote za ushambuliaji, winga zote mbili kushoto na kulia, lakini akimudu kucheza nyuma ya mshambuliaji na mshambuliaji kivuli (False number 9), ametambulishwa jana kwenye mtandao wa Instagram wa klabu hiyo, baada ya tetesi za muda mrefu kuwa nyota huyo angetua Msimbazi.

Gazeti hili hivi karibuni liliripoti habari za Klabu ya Simba kumalizana na mchezaji huyo ambaye awali alikuja nchini kusaini na baadaye akaondoka kurudi kwao Cameroon.

Mchezaji huyo ameandika kwenye mtandao wake wa instagram akiwashukuru kabla ya jana kutangazwa rasmi, ambapo wanachama na mashabiki wa klabu hiyo walionyesha mapokezi mazuri kwake kupitia mitandao ya kijamii.

Kabla ya kutangazwa mchezaji huyo, rais wa Heshima wa Klabu hiyo, Mohamed Dewji, aliandika kwenye mtandao wake wa 'twitter' maneno yafuatayo kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo. "Wanasimba, tulieni, kwa uwezo wa Mungu mambo mazuri yanakuja."

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo,

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042